ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID - SPIKA

1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais

20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
38. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
41. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
44. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu

53. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Thelathini na Mbili – Tarehe 21 Juni, 2017

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika, (Mgeni Hassan Juma) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha hati mezani hotuba ya kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti Bora ya Usimamizi wa Ushuru wa Stempu na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo…

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri, kwanza tuna taarifa ya Spika ambayo inasomwa ni swali ambalo liliulizwa na Mhe. Omar Seif Abeid kuhusiana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Kwanza utaisoma halafu baadae ndio kwa utaratibu ambao tumejipangia samahni ni swali la Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Mhe. Waziri naomba ukae kwanza.

Waheshimiwa Wajumbe, mtanisamehe kwa kuwa taarifa hii ilikuwa haipo mezani kwangu, kwa hiyo sasa nimepata taarifa nyengine. Sasa namuomba Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba na Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora aje asome jibu la swali la nyongeza lilioulizwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Mheshimiwa karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, wakati ninajibu swali Nam. 98 juu ya siku ya mwaka mpya wa Kiisalmu kuwa ni siku ya mapunziko, niliulizwa swali la nyongeza na Mhe. Jaku Hashim Ayoub aliyetaka kujua ni makundi gani yaliyoitwa kutoa maoni yao na ni makundi mangapi ambayo bado hajatoa maoni yake.

Mhe. Naibu Spika, makundi yaliyoweza kutoa maoni yao kwa kukubali moja kwa moja kwamba siku ya mwaka wa Kiislamu iwe ni siku ya mapunziko ni Baraza la Maulamaa la Zanzibar, Walimu wa Madrasa na Maimamu.

Mhe. Naibu Spika, makundi yaliotajwa hapo juu ndio yaliyopangwa kwa sasa kutoa maoni yao kulingana na hali ya fedha, na pindi hali ya fedha itakaporuhusu tutapanga kukutana na makundi mengine kwa ajili ya maoni zaidi. Ahsante.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha hati mezani hotuba ya kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti Bora ya Usimamizi wa Ushuru wa Stempu na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo na Kufuta Sheria ya Ushuru wa Stempu Nam. 6 ya Mwaka 1996.

Mhe. Naibu Spika, naomba pia kuwasilisha hati mezani hotuba ya kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kuweka Vifungu vya Uanzishaji wa Kodi itakayojulikana kama Ushuru wa Bidhaa na Huduma kwa Bidhaa na Huduma zinazoingizwa na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Mohamed Said Mohamed (Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti): Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha hotuba ya Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti Bora ya Usimamizi wa Ushuru wa Stempu na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo na Kufuta Sheria ya Ushuru ya Stempu Nam. 6 ya mwaka 1996.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa naomba kuwasilisha hotuba ya Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Mswada wa Kuweka Vifungu vya Uanzishaji wa Kodi ijulikanayo kama Ushuru wa Bidhaa na Huduma kwa Bidhaa na Huduma zinazoingizwa na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Kwa heshima kubwa sana naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 165

Utaratibu wa Kuwekeza kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (*ZSSF*)

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:-

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (*ZSSF*) ni chombo kichohitaji kuendeshwa kibiashara kwa ajili ya kuwanufaisha wanachama wake ambao wengi wao ni Wanzanzibari.

(a) Je, mfuko huo una mpango gani wa kuanzisha Benki au *SACCOS* zitakazotoa mikopo kwa wajasiriamali hasa baada ya kustaafu.

(b) Je, *ZSSF* inafikiria kuanzisha miradi mikubwa ya kununua boti za uvuvi wa kisasa ambazo pamoja na kuongeza kipato kwa mfuko lakini pia itatoa ajira kwa vijana wetu.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, naomba kujibu swali namba 165 la Mhe. Mwakilishi lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, lengo la kuanzishwa *ZSSF* ni kutoa hifadhi kwa wanachama wake wanapofikia umri wa kustaafu au wanaopatwa na majanga ambayo husitisha au kupunguza kipato kutokana na sababu mbali mbali zisizoepukika ikiwemo ulemavu, maradhi au kifo. Aidha, mfuko umekuwa ukitoa huduma mbali mbali za kuwawezesha wanachama wake ikiwemo mafao ya uzazi ambayo hupatiwa kina mama ambao ni wanachama wa mfuko baada ya kujifungua. Uanzishaji wa benki una utaratibu wake na misingi tofauti ya biashara baina ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na benki. Aidha, *SACCOS* ni taasisi ya kuweka na kukopa inayoanzishwa na wananchama wanaojiweka

pamoja, naomba nimjuilishe tu Mhe. Mwakilishi kwamba Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa sasa hauna dhamira ya kuanzisha benki na hauna sifa ya kuanzisha *SACCOS* kwa sababu hayo ni masuala mawili tofauti.

(b) Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni serikali imeanzisha Kampuni ya Uvuvi (*ZAFICO*) inayolenga kushajiisha uvuvi wa bahari kuu, na ambayo kampuni hiyo inamilikiwa na Mashirika ya SMZ yakiwemo Shirika la Bandari, Shirika la Bima na Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*). *ZSSF* inatarajia kuwa ndio mwenye hisa mkuu wa kampuni hiyo ikiwekeza asilimia 45 ya mtaji wa kampuni hiyo. Uwekezaji katika sekta ya uvuvi utahusisha ununuzi wa boti za kisasa zenye uwezo wa kuvua katika bahari kuu, ujenzi wa kiwanda cha kusindika na kuhifadhi samaki. Uwekezaji huu unatarajiwa kuongeza mapato kwa *ZSSF*, serikali na kutoa ajira kwa vijana wazalendo wa nchi yetu.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Mhe. Waziri kwanza nikupongeze sana kwa majibu yako lakini kama tunavyojua Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ule umiliki wake ni sehemu ya wale wachangiaji ambao ni wadau wakubwa katika umiliki wa ule mfuko. Je, katika uwekezaji tumesikia kuna uwekezaji wamewekeza Kariakoo, wamewekeza hapa ulipojengwa Mnara wa Miaka 50. Je, kuna utaratibu gani uliowahusisha hawa wenye mtaji katika kufanya maamuzi ya uwekezaji ule.

b) Wanafaidika vipi pamoja na kuwa hawakuhusishwa katika uwekezaji ule na ukizingatia ile fedha wao ni wahusika wakubwa kwa sababu ni wachangiaji. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, kwanza tufahamu kwamba mfuko huu umeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Kuanzisha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, na hivi karibuni tumepitisha sheria hiyo mpya ambayo ni Sheria ya Kuanzisha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya Mwaka 2016, ndani ya sheria ile kuna maelekezo ya kisheria jinsi ya uendeshaji wa mfuko huu. Mfuko huu una Bodi ya Wadhamini ambao ndio wasimamizi na waliokabidhiwa na ndio wafanyaji maamuzi ya jinsi ya kuziwekeza fedha hizi kwenye maeneo yenye tija yatakayoweza kukuza mfuko huu kwa ajili ya kulipa mafao ya wanachama pale wanapofikia stahili za kulipwa mafao hayo. Kwa hiyo, wanachama hawashirikishwi katika maamuzi ya uwekezaji, lakini maamuzi yanafanywa kupitia wasimamizi wa mfuko huu ambao ni Bodi ya Wadhamini.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kuniona. Mhe. Naibu Spika, na mimi ningependa nimuulize Mhe. Waziri swali dogo tu moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

a) Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa nchi yetu tuna visiwa viwili vikubwa ambavyo ni Unguja na Pemba na tunategemea sisi katika mkakati wetu tumeangalia masuala ya kiuchumi kwa kukuza uchumi wetu kuangalia eneo la biashara, huduma pamoja na utalii pia. Sasa mimi namuuliza swali moja Mhe. Waziri ni utaratibu gani labda wameufanya au ni

feasibility study gani wameitumia katika kuendeleza Shirika la *ZSSF* kwa kuangalia ukanda wa kuunganisha kibiashara baina ya Pemba, Kenya na Tanzania Bara au Tanga au tunaita the *triangular trade route*.

b) Kwa upande wa *ZSSF* ni uwekezaji gani ambao wamefanya katika sekta ya utalii hasa ukizingatia wafanyakazi wengi ambao wanachangia katika mfuko huu pia wanatokana katika njia moja au nyengine kwenye sekta hii mama ya utalii. Sasa wao kama taasisi wamepanga njia gani za kuchangia au kueleza sekta hii kwa miaka ya hivi sasa na miaka ijayo. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Mwakilishi arudie lile la mwanzo.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Simai Mohammed Said rudia swali lako.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, swali mama linazungumzia kuhusu uchumi na *opportunity* ambazo *ZSSF* wanaweza kuzitumia kueleza mfuko wao na kuna nafasi kubwa sana *ZSSF* wakaitumia baina ya Tanga pamoja na Kenya na Kisiwa cha Pemba. Je, kwa upande wa mfuko wamefanya *feasibility study* gani katika kuuendeleza mfuko huu au kuangalia *opportunities* ili kutumia hiyo *opportunity* ya *triangular trade* ambayo baina ya Tanzania Bara, Tanga, Pemba na Kenya. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Kwanza nimueleze kwamba Mfuko wa Hifadhi ya Jamii umefanyiwa tathmini zaidi ya mara tatu na wataalamu wa kimataifa. Tathmini hizo zililenga kuangalia *investment* ambazo zimeshafanywa sasa hivi, lakini vile vile kuangalia uhimili wa mfuko huu wa kuja kuweza kulipa mafao ya uzeeni *on longer term period.* Hayo yalifanyika na tathmini hizo ziligundua kwamba mfuko huu usipofanyiwa marekebisho ukifika mwaka 2025 ungeweza mfuko wetu ku-*collapse* kwa maana sasa mfuko usingeweza kujiendesha. Sasa kufuatana na tathmini hizo na *investment* ambazo sasa zipo, lakini vile vile kuna *investment guide* ambayo imetayarishwa ndio inayoelekeza mfuko maeneo gani ya kuwekeza. Kwa sasa hivi katika tathmini iliyofanyika hakujakuwepo na mpango wa kuwekeza katika hiyo *triangular trade route* aliyoizungumza Mhe. Simai.

Lakini walichokifanya sasa hivi na maelekezo ya mfuko yalivyo, kwanza ni kuwekeza katika masoko ya fedha lakini vile vile kuekeza katika *realist* na kama mnavyoona wanafanya katika masuala ya ujenzi wa nyumba ambazo zitawanufaisha wanachama wa mfuko huu. Lakini na sasa kama nilivyoeleza wanaekeza katika uvuvi wa bahari kuu kwa kuwa na *share* katika kampuni ya uvuvi. Sasa hilo kama likionekana huko mbele kwamba kuna fursa ya kuekeza katika eneo hilo, basi mfuko nao hautosita kwa sababu lengo lake ni kuhakisha kwamba inawekeza katika maeneo yenye tija itakayohakikisha kwamba mfuko huu unakuwa endelevu.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri katika majibu yako umesema kwamba *ZSSF* wanatarajia kununua boti za uvuvi. Kwanza niseme ni jambo zuri sana kwa sababu vijana wetu wengi watapata ajira kupitia sekta hii ya bahari, lakini nataka kujua ni boti ngapi za uvuvi zinatarajiwa kununuliwa na kwa kila boti inatarajiwa kuchukua watu wangapi wa uvuvi.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Kwanza nilisema kwamba kumeundwa Kampuni ya Uvuvi (*ZAFICO*), na iliyounda ni serikali ilifanya maamuzi ya kuundwa kwa kampuni hiyo. Lakini kampuni hiyo ina wana hisa wake na wana hisa hao ni mashirika yetu likiwemo Shirika la Bandari, *ZSSTC* na pia *ZSSF*. Na nikasema kwamba *ZSSF* ndio wenye *share* kubwa katika hao wana hisa wote, asilimia 45.

Lakini miongoni mwa mambo ambayo wanataka kufanya kama kampuni na sio kama *ZSSF* ni ununuzi wa boti za kisasa za kuvua katika uvuvi wa bahari kuu. Lakini vile vile watajenga Kiwanda cha Usarifu lakini pia na huduma za uhifadhi wa samaki. Hizo ndio kazi ambazo wamejipangia kufanywa na kampuni hiyo. Kwa sasa hawajajua ni boti ngapi zitanunuliwa lakini vile vile katika utaratibu wa kutafuta na wawekezaji wengine bado wanakaribisha *jointventure* na makampuni mengine yatakayoingia na kampuni hii ya kizalendo kuekeza katika eneo la bahari kuu. Kwa hivyo, idadi ya boti zitakazonunuliwa kwa sasa bado hatujazijua.

Nam. 135

Ununuzi wa Mashine za Kutoa Risiti (*EFD Machine*)

(Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 178

Kuundwa Chombo Maalumu cha Utumishi kwa Walimu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Katika utumishi wa umma wafanyakazi wa kada tofauti wamekuwa na taasisi zao za utumishi kama vile Tume ya Utumishi ya Serikali, Idara Maalumu, Baraza la Wawakilishi na Mahakama. Kada ya Ualimu ambayo ni miongoni mwa eneo lenye wafanyakazi wengi nalo limeachwa bila kuwa na chombo chake cha utumishi kama ilivyo kwa baadhi ya nchi jirani.

Je, serikali ina mpango gani wa kuunda Tume ya Utumishi wa Walimu ili shughuli zote za utumishi zinazowahusu walimu ziwe na chombo chake kuzishughulikia.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 178 kama ifuatavyo:-

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inalifanyia kazi wazo la kuundwa kwa Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kuzingatia mazingira halisi ya nchi yetu. Kumekuwa na mapendekezo ya kuundwa kwa chombo hicho kwa walimu, lakini pia kumekuwa na mawazo ya kuundwa kwa Tume ya Utumishi wa kada nyengine kama vile ya madaktari na wauuguzi. Kwa nchi ndogo kama yetu kuwa na utitiri wa Tume za Utumishi kunaweza kuwa na muundo wa gharama kubwa bila ya sababu za msingi. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na vyombo vyengine vya serikali itazingatia wazo la kuundwa kwa chombo cha utumishi wa walimu kwa kufanya uchunguzi wa kina. Pindipo itaonekana chombo hicho kitakuwa na tija, wizara itaishauri serikali kuundwa kwa chombo hiki.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika ahsante sana, nimekuwa nikipokea mara nyingi tu mazowea kutoka kwa serikali, mara tuko mbioni matunda yake tu, na hili wazo litachukuliwa ndio mara nyingi majibu ya serikali. Tuko mbioni, wazo lako tumelichukua, mara tu, wakati huujui. Wizara inalifanyia kazi wazo hili la kuundwa kwa Tume ya Utumishi kwa kuzingatia mazingira halisi ya nchi. Je, ni lini wazo hili litakamilika, mwezi huu, mwakani, baada ya miaka mitatu, ambapo walimu huku wakiendelea na majukumu yao hawajui pa kulalamika kupeleka matatizo yao.

La pili Mhe. Naibu Spika, uchunguzi huu wa kina unahitaji shilingi ngapi ili ukamilike.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Napenda Mhe. Jaku aelewe kwamba, suala la kuundwa kwa tume ya utumishi ya walimu ni suala ambalo linatokana na tamko la sera yenyewe ya elimu. Si maombi yake wala si mapendekezo yake linatokana na sera ya elimu. Katika sera ya elimu kuna matamko mengi ambayo wizara inatakiwa iyafanye, moja wapo ikiwa ni hili la kuunda Tume ya Utumishi. Lakini wizara kwa kuzingatia vipaumbele vyake ikaona kwamba ni vyema kuanza kutekeleza hayo ambayo yametekelezwa. Lakini pamoja na hilo, suala hili tunasema tumeshaanza kulifanyia kazi kwa kuangalia Tume za Utumishi za nchi nyengine zinafanya kazi vipi, zina changamoto gani, zina mafanikio gani na masuala mengine kama hayo. Sasa baada ya kukamilisha uchunguzi huo na tukajiridhisha tutaishauri serikali kuanzisha tume hiyo.

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Naibu Spika, ningependa kuuliza swali dogo tu katika suala la utumishi. Labda Mhe. Waziri angenambia je, ana mpango wowote kwa kuwa walimu wetu wanatumia sana wakati mwengine usafiri wa njiani kwa kutumia magari ya *public* au ya kawaida, wengine wana gari binafsi, lakini wakati mwengine unashindwa kuwatambua katika maeneo mengi kama hawa ni walimu.

Je, serikali ina mpango wa kuanzisha *uniform* rasmi kwa ajili ya walimu wetu ili kuwatambua pale wakati wowote walipo kama ni watu wenye heshima zao, wenye kazi yao na fani zao. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Simai Mohamed Said swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa sasa Wizara ya Elimu haina mpango wa kuanzisha sare kwa walimu badala yake Wizara ya Elimu ina madokezo ambayo imetoa kwa walimu namna ambavyo wanapaswa kuvaa, wanatakiwa wavae mavazi ya heshima kwa sasa bila ya sare.

Nam. 100

Maendeleo ya Ujenzi wa Nyumba ya Daktari Makunduchi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Wananchi wa Makunduchi kwa nguvu zao wamejitahidi kujenga jengo la nyumba ya daktari yenye vyumba sita, ambayo hatua iliyofikiwa ni kuezekwa, lakini imesita kutokana na kukosekana kwa rasilimali fedha na wananchi nguvu zao zimefikia hapo.

Je, ni lini serikali itaunga mkono nguvu za wananchi wa Makunduchi kumalizia ujenzi wa nyumba hiyo ya daktari katika hatua ndogo iliyobakia.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika ahsante, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa wananchi swali lake Nam. 100 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Kwanza kabisa kwa niaba ya wizara yangu napenda nichukue fursa hi kuwapongeza sana wananchi wa Makunduchi, wafanyakazi wa hospitali ya Makunduchi, pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Kusini kwa mashrikiano uelewa na jitihada zao za kujitokeza kuweza kulenga nyumba ya wafanyakazi kwa dhamira ya kupunguza tatizo la makaazi na kuweka utulivu kwa wafanyakazi wa hoslipati hio.

Mhe. Naibu Spika, Nyumba hii iliyojengwa kwa nguvu za wananchi ambayo ina uwezo wa kuishi familiya mbili ni muhimu sana kwa kuwasaidia wafanyakazi kuweza kutoa huduma bora kwa wakati muwafaka. Hivyo basi, wizara yangu haina pingamizi hata kidogo kuunga mkono juhudi za wananchi mara itakapokabidhi ujenzi huu kwa wizara. Wzara itashirikiana kwa karibu na kuona azma ya serikali ya kuleta huduma bora na karibu kwa wananchi inafanyikiwa. Tunawaomba wahusika kufuata taratibza kukabidhi ujenzi huu ili wizara kupitia Idara ya Huduma za Hospitali iweze kuweka mipango ya kukamilisha ujenzi huo. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri kuwapongeza wananchi wa Makunduchi lakini mdomo tu si nyumba ya maneno, naomba kumuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Alipokuwa akijibu Mhe. Naibu Waziri swali la msingi amesema ujenzi huu uko kwenye dhamana yao, kama kweli uko kwenye dhamana yao mbona hakuna harufu yoyote waliyoichukua mpaka muda huu na wananchi wa Makunduchi wakiendelea kuteseka. Hilo la kwanza.

Wananchi wa Makunduchi pamoja na Paje kwa vile juzi tu, tumepitisha bajeti yetu ni lini ujenzi huu utakamilika kama kweli amesema kuwa jengo hili ni muhimu. Tumepitisha bajeti juzi tu na wananchi wanatarajia matarajio, kama kweli muhimu kwa vitendo sio mdomo tu, lini utakamilika ujenzi huu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba nimjibu Mhe. Jaku Hashim maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo. Mheshimiwa kwa utaratibu wa wizara hatuwezi kukamilisha jengo lililoanzwa na wananchi kwa nguvu zao bila ya wananchi wenyewe kufikia hatua na kutukabidhi ili tuendelee kulimalizia. Kwa hivyo, tunawaomba wananchi wa Makunduchi wafuate taratibu watukabidhi lile jengo ili wizara iweze kulimalizia.

Mheshimiwa swali la pili kwamba siku zote hizo kwa nini hatujalimalizia ni kwa sababu moja tu kuwa wananchi wenyewe tuliona wana uwezo wa kuliendeleza kwa hiyo tuwaache waendeleze mpaka watakapofikia baadae watukabidhi ili tulimalizie. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana nami nashukuru kwa kunipa nafasi japo ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri lakini kuna swali dogo nataka kumuuliza. Kwamba wananchi iwapo kama hawajakabidhi lile jengo hawawezi kuliingilia. Je, anakumbuka kwamba tulikwenda Birikau mimi na yeye kituo cha afya cha Birkau kimejengwa huu ni mwaka wa 15 na wananchi wakamwambia kwamba hiki kituo cha afya kimalizike. Je, ni lini kituo kile cha afya kitamalizika.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, ni kweli nilifika katika kituo cha Birikau na nikaona hatua ambayo imefikiwa na kama anakumbuka Mheshimiwa siku ile tulikubaliana kwamba wananchi wenyewe kwanza wakae wamalizie na tukatoa maelekezo kwamba wafikie katika hatua fulani baadae watukabidhi, Mheshmiwa hajanipa *feedback* ya safari ile. Namuomba arudi kwenye kituo chake cha Birikau akae na wananchi wake kama tulivyokaa nao siku ile aone wamefikia hatua gani baadae naomba tuonane ili tujue tunakamilisha kuanzia hatua gani.

Mhe. Naibu Spika, wizara mikono yake iko wazi kumaliza na ku- *support* nguvu za wananchi zisipotee, tuko tayari kumaliza jengo lile.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kuhusiana na makaazi hasa katika masuala ya nyumba za madaktari. Mhe. naibu Spika, kwa kuwa visiwa vyetu tuna maeneo na vijiji tofauti katika sehemu mbali mbali Unguja na Pemba na kumekuwa kuna taasisi ambayo inaitwa *'Zanzibar Outreach Program'*, ambao wamekuwa wanaweka kambi katika maeneo tofauti ya visiwa vyetu hasa katika kutoa huduma tofauti kama *ENT* ambayo ni *Ear, Nose na Throat* pamoja na *checking* nyengine.

Kwa nini serikali haiangalii kwanza makazi haya ambayo ni *Mobile Clinic* hasa za madaktari pamoja na kutoa huduma, ili kuhakikisha vijiji vingi hasa kwa mfano Kisiwa cha Uzi, maeneo

mengine yaliyoko Kaskazini na Kusini mwa Unguja na Pemba, ili ziweze kufikia hizi huduma hasa kwa wazee na akinamama katika maeneo tofauti. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba nilichukue swali hili kama ni ushauri wizara tukae tuangalie uwezekano, na kwa kweli ni suala zuri linaweza likasaidia kuwafanya wenzetu waendelee kutusaidia katika nyanja mbali mbali. Nakushukuru na tutalichukua na tutakaa tulizungumze tupange na naamini kwamba muwafaka utapatikana. *(Makofi)*

Nam. 46

Malipo ya Kodi kwa Madereva wa Bodaboda

Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Aliuliza:-

Pamoja na azma nzuri ya serikali katika kuwatumikia wananchi wake katika shughuli mbalimbali ikiwemo kuridhia usafiri wa bodaboda kutumika kwa kusafirisha abiria sehemu mbalimbali ndani ya maeneo yetu hapa Zanzibar.

(a) Je, hatuoni kuwa tumeipunguzia serikali mapato katika upande wa kodi ambazo zilikuwa zinalipwa na wamiliki wa gari za abiria (*Taxi)* ambazo sasa zimepungua kutokana na uwepo wa bodaboda.

(b) Je, ni gharama au kodi gani wanazolipa wenye bodaboda ili kuishawishi serikali iridhie kutoa huduma hii.

(c) Je, serikali haioni kuwa hawawatendei haki wenye *Taxi*.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 46 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, serikali kama nilivyojibu hivi karibuni haijaruhusu vyombo vya maringi mawili kusafirisha abiria kwa ajili ya biashara nyengine yoyote isipokuwa ile ya kukodi na kuendesha mtu yeye mwenyewe.

(a) Serikali, haijapunguza mapato kwa sababu vyombo vyote vya moto vinalipa gharama kulingana na aina ya chombo na biashara anayoifanya.

(b) Wenye vyombo vya maringi mawili wanalipia gharama za matumizi ya njia na gharama za ukaguzi na walioruhusiwa kufanya biashara wanalipia leseni ya biashara.

(c) Serikali inawatendea haki wale wote ambao wanafanya biashara kwa kuwawekea utaratibu maalum kulingana na aina ya biashara zikiwemo *TAXI*. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana, pamoja na majibu yenye mchanganyiko ya Mhe. Naibu Waziri, juzi alijibu swali hilo kutokana na sheria ya mwaka 2003 Nam. 7 na leo kanijibu tena. Naomba anambie ni biashara gani waliyoruhusiwa chombo cha maringi mawili kwa mujibu wa majibu yake hapa, amesema kwamba wameruhusiwa leseni wafanyabiashara wanalipia leseni ni biashara gani bodaboda ilioruhusiwa.

Pili, je, haoni kwamba kutokana na uhaba wa ajira wakatunga sheria ili kuviruhusu vyombo vile ikawa rasmi na kutoa ajira nyingi kwa watu wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo. Kwa mujibu wa sheria yetu Nam. 7 ya mwaka 2003 kifungu 48 kimetaja aina zote za vyombo ambavyo vinaruhusiwa kufanya biashara, vyombo vya maringi mawili havijatajwa isipokuwa tumesema kwa wale wanaokwenda kukodi au kuendesha wenyewe. Kama nilivyosema sisi serikalini tumelifuatilia sana hili suala, tumewatuma wataalamu wetu kwenda kuangalia Bara jinsi ajali zinavyotokea kule kutokana na biashara hii ya bodaboda na vile vile tunaangalia afya za watumiaji wale wanaopakiwa kusema la kweli hii kazi inataka utafiti na sisi tunaendelea na utafiti. Lakini napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi aliyeuliza swali hili kwamba, kwa mujibu wa kifungu kile cha 48(4) Waziri anao uwezo wa kuongeza leseni yoyote pale anapoona baada ya kushauriana na mamlaka husika inaweza kufanya hivyo.

Kwa hivyo, tunalichukua tutalifanyia kazi lakini tunalifanyia kazi kwa maslahi ya watu wetu na vile vile kuepusha ajali ambazo hivi sasa zinaongezeka siku hadi siku na hasa hivi vyombo vya maringi mawili. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Naibu Spika, nashukuru na mimi kwa kunipa nafasi hii, awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema mwenye kurehemu aliyeumba mbingu na ardhi na vilivyomo vyote kwa kutujaalia kufika hapa salama usalimini.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza nimpe pongezi kwa majibu yake mazuri lakini nina swali moja ambalo lina (a) na (b) ambalo niongezee. Kwa kuwa wakati umefika na mabadiliko tumeyaona, tukichukua mfano kama Tanzania Bara wamefanya kila aina ya njia katika sehemu ya bodaboda wameshindikana na sasa hivi polisi wamewafanyia semina na wanawaruhusu katika baadhi ya mambo haya.

(a) Je, serikali haioni umuhimu wa bodaboda zile pikipiki zao kuzitia rangi maalum na kuzisajili ili kuzielewa waendelee na shughuli hiyo lakini sio mjini iwe ni maeneo ya mashamba ambapo zinasaidia watu.

(b) Kwa sababu hali halisi imeonekana kwamba hawana ajira na wanaonekana vijana wanaendesha mapikipiki ama kwamba wana leseni ama hawana au leseni zao hazikidhi. Haioni kwamba kuna haja ya kuwafanyia semina mabodaboda hawa kupunguza ajali.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Kama nilivyosema sisi wataalamu wetu wameshakwenda Dar es Salaam kuangalia namna gani kazi za bodaboda wanavyofanya na athari zake na vile vile ni karibuni tu watu walifanyiwa semina wametoka Bara, lakini nawaambia kwa mujibu wa sheria hii basi waziri hatua ya mwisho ndiye atakayeweza kutoa ruhusa au kutotoa ruhusa. Sisi hatutaki kutoa ruhusa kabla ya kufanya utafiti wa kina ili baadae tusijekuwa tunaitumia hii sheria ikaja kuleta madhara zaidi na watu wakapiga kelele baadae tukawa sisi ndio wenye kuwajibika kwa hilo. Kwa hivyo, tumechukua ushauri wake na tutaufanyia kazi. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kuniona na mimi ningependa kumuuliza swala dogo tu la nyongeza lenye fungu (a) na (b).

(a) Kwa kuwa usafiri huu wa boda boda tayari unatumika na wananchi katika kutoa huduma mbali mbali. Ni kiasi gani cha fedha yuko tayari kuondosha katika fungu lake mwaka ujao ili kuhakikisha kwamba wale wote wanaopata ajali za kwenye boda boda wataweza kupata matibabu katika kuanzisha taasisi ya mifupa na wale wanaopata ajali katika Wizara ya Afya hasa Mnazi Mmoja ili *department* yetu *orthopedics* iweze kutoa huduma kwa wale wote wanaopata ajali pamoja na kuvunjika.

(b) Utaratibu gani wa kisheria wanaotumia pale ambapo askari polisi anakamatwa au anakutwa amepanda kwenye boda boda ambapo anatumia huduma hiyo kwa kulipa ili kuweza kufika katika eneo la safari ambayo anayokwenda.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Simai Mohamed Said Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Tunguu swali lake lenye kifungu (a) na (b) la nyongeza kama ifuatavyo:

(a) Kama nilivyosema sheria haijaruhusu boda boda kufanya kazi zao hatujawapa leseni hiyo na naendelea kusisitiza wale wote iwapo watathibitika kwamba wanafanya hiyo kazi bila ya ruhusa basi tutawapeleka mahakamani na ambapo adhabu yake ni faini ya dola isiyopungua 50.

(b) Kama nilivyosema mwanzo sisi tunaendelea kuelezea wazi kwamba hii biashara inataka lazima uangalifu mkubwa sana, tulipoenda Tanzania Bara kwa wenzetu wametwambia nyinyi mnaendelea kufanya kazi nzuri, sisi wenyewe tulioruhusu boda boda tunaona athari yake wakawapeleka wale watu wetu wa leseni na usafirishaji kule Moi na wakaona watu walivyoathirika.

Kama nilivyosema unapoendesha boda boda unatakiwa utumie wenyewe wanasema kofia ngumu. Lakini unaweza kumtoa mtu anaenda harusini akasema ile kofia chafu akipata ajali kosa vile vile kwa sababu hajavaa *helmet.* Lakini vile vile iwapo polisi yoyote atatumika katika kupanda boda boda basi polisi wenzake watatakiwa wamchukulie hatua

na hilo litakuwa kosa la nidhamu kwa sababu wao ndio watu wa mwanzo wanatakiwa wazifuate hizi sheria zetu. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mheshimiwa, Waheshimiwa Wajumbe naomba mpunguze minongono sauti zinaingiliana...

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu utaratibu Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub nazungumza mimi. Sauti zinaingiliana naomba sana mpunguze minongono, ili tupate kusikilizana humu ndani Waheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu utaratibu Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Haya Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kuhusu utaratibu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante nimesimama Kanuni ya 63 sijui utanihitaji nisome kuhusu utaratibu au niendelee kunako hoja yangu iliyonisimamisha hapa 42,43.

Mhe. Naibu Spika: Ni kuhusiana na nini?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: 42 Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Hatujamaliza Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Hatujamaliza maswala na majibu naomba utuachie kwanza tumalize halafu tutaendelea na hoja ambazo unataka kuzileta. Tunaendelea na Mhe. Suleiman Sarahan Said.

Nam. 109

Matumizi yasiyo Rasmi ya Barabara

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza**:**

Zanzibar ni nchi moja wapo inayokuwa kwa kasi kimaendeleo na hivi sasa katika sekta za usafiri kama gari zimekuwa nyingi sana. Hata hivyo, ongezeko hilo la gari limeleta changamoto ambapo gari hizo hulazwa barabarani na kusababisha usumbufu ambapo hata kupita inakuwa shida na ajali kuongezeka.

(a) Je, serikali hailioni hilo, na kama imeliona, imechukua hatua gani ili kuepusha hatari.

(b) Ni lini serikali itapiga marufuku vitendo vya kulaza gari barabarani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu**:**

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swala lake Nam. 109 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli Zanzibar kumekuwa na ongezeko kubwa la gari na baadhi yao hulazwa barabarani na zinasababisha njia kuwa nyembamba.

(a) Serikali inaliona hilo na Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na manispaa husika imeanza kuzichukulia hatua gari zote zinazolazwa katika barabara.

(b) Seriakli tayari ishapiga marufuku vitendo hivyo na Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na manispaa husika zitaendelea kuwachukulia hatua kali wale wote wanaojaribu kulaza gari katika barabara. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, na mimi nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nina suala (a) na (b) la nyongeza:

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa mjini ndio nyumba huwa nyumba zina ghorofa na watu wanakuwa wengi ambao wanakaa kwenye ghorofa na kila mmoja pengine anakaa na gari na ni halali yake mtu kukaa na gari katika nyumba yake wakati eneo lile hapana.

(a) Je, ana mpango gani wa nyumba ambazo zitajengwa za kisasa za kuilazimisha nyumba hiyo ijengwe *underground* kwamba gari ziweze kupaki chini ya mvungu wa nyumba.

(b) Ni mara ngapi umefanya upereshen ya kulaza magari barabarani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Chake Chake masuala yake ya nyongeza yenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kama unavyojua tuna Mji Mkongwe ambao ule kutokana na hali yake ya kuwa katika uhifadhi wa *UNESCO* ule hatuwezi tena kuubadilisha ndio mjini mfano na vile vile majumba yaliojengwa ya maendeleo ya Michenzani ziko sehemu ambazo watu wanaweza kupaki gari hasa jumba namba 10. Lakini licha ya hivyo kwa hivi sasa hasa katika mpango wetu huu wa *Darajani corridor* basi kutakuwa na sehemu maalum za kupaki gari na sehemu hizo zitasaidia sana kwa watu wa mjini na wengine wote ku-*park* gari zao huku kwa hiyo kupunguza ule msongamano na uwepo wa magari ndani ya mji wetu.

(b) Kama nilivyosema hapo mwazo kwamba sisi tuko karibu sana na Jeshi la Polisi na zaidi napenda kumpongeza sana Kamanda Mkadam ambaye kila wakati tunawasiliana na ninapo mpa maagizo huyafuata. Kwa hiyo, hili zoezi hadi hivi sasa tunaendelea nalo na ni zoezi endelevu na sisi tutachukuwa hatua kwa wale wote wanaolaza gari barabarani. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kuniona. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa kila kukicha engezeko la magari kutokana na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa usimamizi mzuri unaofanywa kuongeza maisha bora ya Wazanzibari na Watanzania kwa jumla kitu ambacho kinachopelekea Wazanzibari wengi kununua magari tafauti makubwa na madogo ambayo yatazidi kuongezeka.

(a) Katika kuleta angalau afueni kupunguza magari barabani mbali ya maegesho. Je, serikali imefikiria kuanzisha mabasi kwa ajili ya kutoa huduma za abiria tofauti hasa wanaotaka kuingia mjini na kutoka.

(b) Kwa kuwa kama majibu aliyoyatoa Mhe. Waziri awali upande wetu sisi mara nyingi serikali katika nchi tafauti huwa wanatoa afueni hasa katika masuala la *incentive* kwenye *tax* na wale ambao wafanyabiashara watakaojitokeza kujenga maghora ambao watakuwa na huduma za kutoa maegesho ya magari yawe kwenye ghorofa zao.

Je, serikali yetu imejipangaje kutoa huduma ya unafuu katika *incentive* hizi kwa wafanyabiashara ili waweze kuekeza hasa katika maeneo ya miji mipya kama Tunguu pamoja na Jumbi ili kupunguza msongamano wa magari katika mitaa. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Simai Mohamed Said Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Tunguu masuala yake la nyongeza yenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Wizara tuko katika mpango mkakati wa kutaka kuhakikisha kwamba tunakuwa na usafiri wa umma na nina imani kubwa sana utakapoanza usafiri utachunguza vile vile msongamano wa magari na magari mengine kama ulivyofanywa utaratibu Dar es Salaam tutaangalia njia maalum za kwenda.

(b) Mhe. Naibu Spika, kuhusu uanzishaji au kuwashirikisha watu katika kuanzisha nyumba na vile vile kuweka sehemu za *parking*. Napenda kumuhakikishia kwamba ni wazo zuri na sisi tunaomba sana wale ambao wawekezaji watakuja Fumba wameanzisha hivi sasa hivi katika mpango anaojenga ndugu Bakhressa muwekezaji wetu na nina imani na wawekezaji wengine wakija kutokana na mipango miji na wana vijiji wetu wao wataiga mfano huo. Ahsante sana Mhe. Naibu.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri kwa kuwa maendeleo siku zote yana faida yake na hasara yake. Pamoja na kwamba swali mama linazungumza kwamba magari mengi yanalala barabarani hii ni sehemu ni kwamba magari yapo yamekuwa mengi. Lakini Mhe. Waziri je, unajua kwamba magari ambayo kuwa sasa hivi yanabeba mzigo wa mawe barabarani katika harakati za kujijengea maendeleo nchi yetu yanaleta hasara kwa kupakia mawe yale mpaka kuipita bodi ya magari na kusababisha mawe yale kuanguka na suala hili nililifatilia na nikazungumza na watu wa *traffic* wakasema hawajapewa sheria ya kuweza kuwakataza.

Je, utachukuwa hatua gani katika kuzuia upakiaji mbaya ule wa mawe kama vile mlivyochukuwa hatua ya kuzuia mchanga kuyafunika. Ni hatua gani mtachukuwa kuzuia upakiaji mbaya wa mawe ambao kuwa unasababisha hatari kwa walioko chini ya barabara. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji napenda kumjibu Mhe. Shehe Hamad Mattar Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Mgogoni suala lake kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema hapo mwanzo kila magari ya mizigo yamepangiwa kwa mujibu wa uzito wake kuna leseni tunazitoa kwa magari yasiyozidi uzito wa kilo 3500 na vile vile na zaidi ya 3500. Kwa hiyo, iwapo gari yoyote itazidisha uzito au hata abiria ni wajibu wa polisi kuisimamisha gari ile ba baadae kuipeleka kituoni na baadae kuichukulia hatua kwa wale wote ambao wataenda zaidi ya ule utaratibu wetu wa kuchukuwa mzigo ulivyowekwa.

Kwa hivyo, sisi wakati wowote tunaomba sana wananchi wasisubiri polisi kwa sababu baadhi ya wakati polisi wanakuwa hawapo katika yale maeneo. Lakini na wao wakiona hivi sasa tuna ubalozi wa Usalama barabarani na wananchi basi wapige simu polisi ili polisi wafike lile eneo kuisimamisha ile gari na kuichukulia hatua kwa kuwapeleka mahakamani wale wote wanaozisha uzito zaidi na ule uzito unaotakiwa kwa mujibu wa gari husika. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushukuru kwa kuniruhusu nimesimama kuhusu utaratibu kifungu 42 hoja ya kujadili jambo la dharura. Naomba nikisome Mhe. Naibu Spika.

'Baada ya muda wa maswali kuisha Mjumbe yoyote anaweza kutoa hoja kuwa Baraza liakhirishe shughuli zake zilioneshwa katika orodha ya shughuli ya Baraza na lijadili jambo la dharura muhimu kwa umma na kwa ruhusa ya Mhe. Naibu Spika'.

Vile vile kunako kanuni ya 43 Mhe. Naibu Spika, kauli za Serikali:

'Kiongozi wa shughuli za serikali au waziri yoyote anaweza kutoa kauli katika Baraza kuhusu jambo lolote ambalo serikali inawajibika na baada ya hapo Mwenyekiti wa Kamati inayohusika au Mjumbe mwengine alieidhinishwa na kamati anaweza kupewa nafasi ya kutoa maoni katika hili'.

Mhe. Naibu Spika, kuna jambo limetokea la dharura tena kubwa sana katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja. Kwa masikitiko .....

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, sijakuruhusu kutoa hiyo hoja yako. Umeniomba na ukiomba unasubiri upewe au ukataliwe au siyo. Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Jaku Hashim

Ayoub ana hoja na anataka kuiwasilisha hoja yake mimi nitamruhusu kuiwasilisha hoja na ninamruhusu awasilishe hoja yake. Lakini hoja hiyo haitajadiliwa na nitaomba hoja hiyo aichukuwe Mhe. Waziri akaifanyie tu kazi na kwa sababu tumeshajadili sana humu kipindi cha bajeti, mambo mengi serikali imeahidi kuyafanya. Kwa hiyo, na hili liwe moja katika mambo ambayo ni ya dharura kwa sababu ni dharura na hoja yenyewe ni ya dharura nitamwachia Mhe. Waziri akalishughulikie hilo suala.

Kwa hiyo, naomba Mhe. Jaku Hashim Ayoub uje na hoja yako lakini halitajadiliwa. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa vile nimeomba na ukanipa nakushukuru sana.

Kwa maana hiyo, itakuwa ni kauli ya 43 hiyo serikali kuchukuwa kauli na kuileta. Lakini niombe kabla ya kufungwa Baraza hili Mhe. Naibu Spika, tupate jawabu kabla ya kuakhirishwa Ijumaa.

Mhe. Naibu Spika, kwa unyonge kabisa na kwa hudhuni kubwa Hospitali yetu inayotegemea kuitwa ya Rufaa bado hali tete nimekwenda kushuhudia mimi mwenyewe hii leo asubuhi jana nikafikiri hatua zitachukuliwa. Lakini nimeona jambo moja kidogo zuri kibanda cha Jenereta kinaanza kujengwa sasa hivi.

Mhe. Naibu Spika, lakini *lift* ni kitu muhimu sana katika hospitali ile, mjamzito anapata shida kutaka kupelekwa pale, mgonjwa wa mifupa aliepata ajali hawezi kubebeka akapelekwa kwenye kitengo cha *X-Ray* na *X-Ray* vile vile ni hoi bin taabani.

Lakini mgonjwa aliekuwa mzito wa mwili Mwenyezi Mungu aliemjaalia habebeki kupelekwa kule juu ni sababu gani za msingi karibu miezi miwili mpaka sasa hivi *lift* ile hakuna kinachoendelea hakuna *lift* ya zamani na mpya iliyotiwa na enzi za Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini kipindi kile na serikali siku zote haiogopi kupata kwa wananchi wake ndio majibu ya serikali.

Lakini kama hilo halitoshi vile vile la paa zima lile la hospitali juu mwazo mpaka mwisho linavuja, wagonjwa juzi kulitokea *short* ya umeme ni wagonjwa wakapata *short* na wao walipona wakati huo huo wakateremka chini kutokana na maji ya mvua na umeme havikubaliani.

Kwa hiyo, naiomba serikali kwa unyenyekevu wa hali ya juu *lift* ni kitu muhimu nataka kauli kabla ya Ijumaa Mwenyezi Mungu akitujaalia kuwa hai na uzima nipate jawabu. Ilichukuwe serikali ikalifanyie kazi na Mhe. Naibu Spika, nahitaji msaada wako na Waheshimiwa Wajumbe mnisaidie hili. Hili si langu letu sote na mimi pengine kesho nipate homa nipelekwe pale au Mhe. Abdalla Ali Kombo na mwili wake huu kidogo *mashaallah* hawezi kubebeka kupelekwa juu. Kwa hiyo, nahitaji msaada. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante naamini kwamba serikali imelichukuwa na waziri amelisikia na naamini amelisikia na naamini kwamba waziri atalifanyia kazi. Kwa hiyo, tunaendelea.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti Bora ya Usimamizi wa Ushuru wa Stempu

(Kusomwa kwa mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika....

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri kabla ya kuanza naomba sasa nimpishe Mhe. Mwenyekiti, Mwanaasha Khamis Juma aje aendelee na shughuli hii. Mwenyekiti karibu.

(Hapa Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwanaasha Khamis Juma alikalia kiti)

Mhe. Mwenyekiti: Tuendelee Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, Mswada huu unawasilishwa kwa Hati ya Dharura, hivyo naomba kabla sijaanza kusoma hotuba yangu, kusoma Hati ya Mhe. Rais kama ilivyo na kwa mujibu wa Kanuni ya 80 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2016.

Mhe. Mwenyekiti, Hati hiyo ya Dharura ya Mhe. Rais inasomeka kama ifuatavyo:-

Tangazo nambari 49 Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2016, Shahada ya Mswada wa Serikali wa Dharura chini ya Kanuni ya 80.

Kwa uwezo niliopewa chini ya Kanuni ya 80 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2016, "Mimi Dkt. Ali Mohamed Shein - Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi natamka kwamba Mswada wa Serikali wa Kuanzisha Sheria ya Ushuru wa Stempu ni wa dharura na ni wa haraka sana na kwamba haiwezekani kutimiza masharti ya Kanuni ya 79, imetiwa saini na muhuri wa Rais tarehe 12 Mei, 2017, lipo jina la Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na saini yake. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kusoma hotuba yangu ya kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Ushuru wa Stempu itakayochukua nafasi ya Sheria ya Ushuru wa Stempu Nam. 6 ya mwaka 1996.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa sheria mpya ya Ushuru wa Stempu itakayochukua nafasi ya Sheria ya Ushuru wa Stempu ya mwaka 1996, sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda kurudia tena kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma, kwa mara nyengine tena kutujaalia afya na utulivu uliotuwezesha kukutana katika Baraza hili kwa leo kwa ajili ya kuujadili Mswada wa Sheria mpya ya Ushuru wa Stempu unaosomwa kwa mara ya pili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa na kwa heshima kubwa napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti Mhe. Mohamed Said Mohamed Dimwa, Makamu Mwenyekiti wake Mhe. Bahati Kahati Khamis Kombo, pamoja na wajumbe na makatibu wote wa kamati. Kwa hakika wamefanyakazi kubwa kuupitia mswada huu na kurekebisha kasoro zilizojitokeza, maoni na michango yao imesaidia sana kuweka sura nzuri ya Sheria yetu baada ya kuidhinishwa na Baraza hili Tukufu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia nichukue fursa hii kumshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu na watendaji wake wote kwa msaada mkubwa sana na kazi kubwa sana waliofanya katika kuandaa Mswada wa Sheria hii ninayoiwasilisha hapa leo.

Mhe. Mwenyekiti, kimsingi hivi sasa wafanyabiashara wadogo wadogo hulipa kodi maalum ya wafanyabiashara wadogo, kwa maana ya *presumpt tax* chini ya Sheria ya Kodi ya Mapato inayosimamiwa na Mamlaka ya Mapato (*TRA),* na pia hulipa ushuru wa stempu unaosimamiwa na *ZRB.*

Mhe. Mwenyekiti, chini ya utaratibu huu wafanyabiashara wamelalamikia gharama za ulipaji kwa kutakiwa kulipa kodi katika taasisi mbili tofauti na walilalamikia pia ukubwa wa kodi hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande mwengine ushuru wa stempu hukusanywa katika mauzo yasiyostahiki kulipiwa kodi ya ongezeko la thamani (*VAT)* ama kwa kusamehewa au kwa kutofikia kiwango cha kusajiliwa chini ya *VAT*. Aidha ushuru huo hutozwa katika hati mbali mbali. Maeneo haya nayo pia yamekuwa yakilalamikiwa hasa kutokana na kutokuwa bayana zaidi katika hati.

Madhumuni na Sababu:

Mhe. Mwenyekiti, Mswada wa Sheria ninaouwasilisha unakusudia kuondoa kasoro nilizozitaja na utapelekea kupatikana mambo yafuatayo:-

1. Kupatikana kwa Sheria mpya ya Utozaji wa Kodi wa Ushuru wa Stempu itakayoleta ufanisi katika ukusanyaji wa kodi;
2. Kuimarika kwa usimamizi wa ukusanyaji kodi na kuongezeka mapato ya serikali;
3. Kuingizwa hati na nyaraka zilizokuwa hazikuainishwa katika Sheria ya Ushuru wa Stempu iliopo; na
4. Kuainishwa kwa hati na nyaraka zinazopaswa kutozwa ushuru wa stempu na mtu anayestahiki kulipa ushuru huo.
5. Mhe. Mwenyekiti, faida nyengine zitakazopatikana ni pamoja na kuwepo kwa utaratibu bora zaidi na viwango maalum vya kutozea kodi kwa wafanyabiashara wadogo wadogo wa bidhaa na huduma.
6. Kuwepo kwa utaratibu mzuri wa usimamizi wa ukusanyaji kodi kwa wafanyabiashara waliokuwa hawakusajiliwa katika viwango vya *VAT*.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na faida hizo, Mswada utasaidia wafanyabiashara wadogo wadogo kulipa kodi kwenye taasisi moja tu, kwa maana ya *ZRB*. Baada ya kupitishwa Mswada huu wafanyabiashara hao hawatahitajika tena kulipa na *TRA* kama ilivyokuwa awali.

Aidha, viwango vitakavyolipia ushuru huo chini ya majadweli ya sheria hii vimepunguzwa kulinganisha na kiwango cha jumla wanacholipa sasa kwa *TRA* na *ZRB*. Serikali imechukua hatua hii kusudi ili kuendelea kuikuza sekta binafsi hususan wafanyabiashara wadogo wadogo ambao wote ni wazalendo.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada huu umegawika katika sehemu tano. Naomba kwa ruhusa yako nichukue fursa hii kuziwasilisha sehemu hizo kwa ufupi kama ifuatavyo:-

Sehemu ya Kwanza ya Mswada inahusiana na vifungu vya utangulizi, ambavyo vinaelezea jina la Sheria utumikaji wake, vifungu vya ufafanuzi wa maeneo yaliyotumika katika Sheria hiyo.

Sehemu ya Pili ya Mswada inahusiana na vifungu vya utozaji wa ushuru wa stempu na utawala na sehemu hii inahusu utozaji wa ushuru, hati ya kutokuwa na pingamizi na masuala ya utawala.

Sehemu ya Tatu ya Mswada inahusisha vifungu vinavyoweka masharti ya jumla yanayohusika na hati. Sehemu hii ndio inayoweka utaratibu mzima wa usimamizi, udhibiti na tathmini ya ushuru wa stempu katika hati mbali mbali.

Sehemu ya Nne ya Mswada inaweka utaratibu wa usimamizi wa ushuru wa stempu katika biashara, inaelezea kiwango cha malipo, shughuli zinazotozwa ushuru, thamani ya kutozwa kodi, utambulisho wa walipa kodi, kudhibiti, kutathmini na kukusanya na masuala ya uwasilishaji nyaraka, kwa maana ya *return*.

Sehemu ya Tano inahusu masharti mengineyo juu ya usimamizi wa ushuru wa stempu, ikiwemo kuhusu kushindwa kuonesha maelezo kamili kuhusiana na hati, kusajili nyaraka zilizokuwa hazijawekewa stempu, makosa yanayohusiana na kuweka stempu katika hati, kuondosha stempu, ukwepaji wa ushuru, umiliki usio halali wa stempu, stempu zilizoghushiwa.

Mambo mengine ni pamoja na adhabu za jumla, uwezo wa kuchunguza, uwezo wa kuingia, uwezo wa kusamehe malipo ya ushuru katika hati, kanuni pamoja na kufutwa kwa Sheria ya Ushuru wa stempu ya mwaka 1996 na kuhifadhi mambo yaliyotendeka chini ya sheria hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na sehemu hizo nilizoziainisha Mswada una viambatanisho vya majadweli yafuatayo;

1. Jadweli la Kwanza linahusisha orodha ya hati na viwango vya malipo yake.
2. Jadweli la Pili *return* ya wakala wa ushuru wa stempu na
3. Jadweli la Tatu linatoa mfumo wa malipo kwa mkupuo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia kwa mara nyengine tena naomba kuwashukuru sana Kamati ya Bajeti kupitia Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wake. Naishukuru sana Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kupitia kwa Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Vile vile nawashukuru sana watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kupitia kwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, Waziri wake na Katibu Mkuu wake na kwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa kupitia kwa Katibu Mkuu ndugu Khamis Mussa Omar. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niwashukuru sana Bodi ya Mapato (*ZRB)* na Mamlaka ya Mapato tawi la Zanzibar (*TRA)*. Pia niwashukuru Makatibu wa Kamati wote walioshirikiana na sisi katika kuandaa Mswada wa Sheria.

Pia shukrani zangu za dhati ziwaendee sekta binafsi, ikiwemo Jumuiya ya Wafanyabiashara Wenye Viwanda na Wakulima, wadau na washauri wote walioshirikiana na sisi katika kuandaa dhana ya Mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa sasa nawaomba Waheshimiwa Wajumbe waupokee Mswada huu, waujadili na hatimaye wauidhinishe ili iwe Sheria ya Ushuru wa Stempu itakayoondoa Sheria ya sasa ya Ushuru wa Stempu ya mwaka 1996.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa hotuba yako. Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

Mhe. Simai Mohamed Said (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti): Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kabisa na kwa ruhusa yako naomba sasa kusoma hotuba ya Mwenyekiti wa Kamatiya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi kuhusu mswada wa sheria ya kuweka masharti bora ya usimamizi wa ushuru wa stempu na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu, kwa kutujaalia neema ya uhai na uzima wa afya ili tuweze kutekeleza majukumu yetu katika Baraza letu tukufu. Aidha napenda kukushukuru wewe binafsi, kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako kwa niaba ya Kamati yangu ya Bajeti, ili niwasilishe maoni ya Kamati kuhusiana na Mswada wa Sheria ya Usimamizi wa Ushuru wa Stempu na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa umakini wao na ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu ya Kamati. Naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatvyo:

1. Mhe. Mohammed Said Mohammed — Mwenyekiti
2. Mhe. Bahati Khamis Kombo — Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Simai Mohammed Said — Mjumbe
4. Mhe. Shehe Hamad Mattar — Mjumbe

5. Mhe. Asha Abdalla Mussa Mjumbe
6. Mhe. Abdalla Ali Kombo Mjumbe
7. Mhe. Zulfa Mmaka Omar Mjumbe

Aidha, Kamati yangu ina makatibu wawili ambao ni;

1. Ndg. Abdalla Ali Shauri Katibu
2. Ndg. Kassim Tafana Kassim Katibu

Mhe. Mwenyekiti, Kanuni ya 83(6) inaipa uwezo kamati kualika wadau kwa lengo la kutoa maoni yao kuhusiana na mswada uliowasilishwa mbele ya kamati husika, kamati yangu iliitumia vyema fursa hiyo kwa kualika wadau kutoka taasisi mbali mbali, ili kusaidia uchambuzi na kuufanya mswada huu uwe bora zaidi. Hivyo napenda kuchukua fursa hii, kuwashukuru wadau hao kwa maoni na ushauri wao mzuri waliotupatia.

Uchambuzi wa Mswada

Mhe. Mwenyekiti, Madhumuni ya Mswada huu ni kuliomba Baraza, kufuta Sheria ya Ushuru wa Stempu Nam. 6 ya mwaka 1996 na kutunga Sheria mpya ya Stempu, itakayoweka utaratibu mzuri zaidi wa ukusanyaji na usimamizi wa ushuru wa stempu katika nyaraka, kuongeza hati mpya zinazopaswa kutozwa ushuru ambazo hazikuwemo katika Sheria ya Ushuru wa Stempu ya mwaka 1996, na kufanya marekebisho kwa kuongeza ama kupunguza viwango vya ushuru katika baadhi ya hati.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inaunga mkono uamuzi wa serikali wa kuleta mswada huu, ambao utapelekea ufanisi zaidi katika ukusanyaji wa mapato ya nchi, ambayo yatasaidia katika shughuli mbali mbali za kuwafikishia wananchi huduma za msingi. Aidha, kwa kuwa Mswada huu pia una dhamira ya kuwaondolea wananchi mzigo mkubwa wa kulipa kodi katika taasisi mbili, Bodi ya Mapato ya Zanzibar (*ZRB*) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*).

Mhe. Mwenyekiti, naomba nirudie. Aidha, kwa kuwa Mswada huu pia una dhamira ya kuwaondolea wananchi mzigo mkubwa wa kulipa kodi katika taasisi mbili, Bodi ya Mapato ya Zanzibar (*ZRB*) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), ambapo mswada huu unakusidia kuwaondolea usumbufu huo wafanyabiashara wadogo wadogo, ambapo sasa watatakiwa kulipa kodi Bodi ya Mapato ya Zanzibar (*ZRB*) pekee. Kimsingi Kamati yangu inaunga mkono na imefarajika sana na uamuzi huo wa serikali ambao unaonesha kuwajali walipa kodi.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na uelewa mdogo wa wananchi kuhusu sheria za kodi, kumekuwa na mitazamo mibaya dhidi ya serikali ambapo kila mara inapotokezea kuletwa mswada unaohusiana na kodi au yanapofanyika marekebisho ya kodi, dhana ya wanachi walio wengi ni kwamba serikali inataka kupandisha au kuanzisha kodi mpya.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nirudie tena. Mhe. Mwenyekiti, kutokana na uelewa mdogo wa wananchi kuhusu sheria za kodi, kumekuwa na mitazamo mibaya dhidi ya serikali ambapo kila mara inapotokezea kuletwa mswada unaohusiana na kodi au yanapofanyika marekebisho ya kodi, dhana ya wanachi walio wengi ni kwamba serikali inataka kupandisha au kuanzisha kodi

mpya. Hivyo, kamati yangu inaishauri serikali kutowa elimu ya kutosha kwa jamii, kwa kuwa baadhi ya marekebisho yanayofanywa yanakuwa na lengo la kuwapunguzia mzigo walipa kodi tofauti na fikra za baadhi ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, ili kujenga mazingira rafiki baina ya serikali na walipa kodi na kuepusha kuwakandamiza wafanyabiashara, kamati yangu inashauri, kupewa uwezo Kamishna wa Bodi ya Mapato wa kufanya tathmini ya mauzo ya mlipa kodi na kuweza kumbadilishia kiwango anachopaswa kulipia pale inapotokezea mauzo yake yameshuka.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu pia inaishauri serikali kuangalia uwezekano, kwa wafanyabiashara ambao biashara zao sio kubwa kulipia kila baada ya miezi mitatu, badala ya kulipia kila mwezi.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu imeupitia mswada huu kifungu kwa kifungu na kupendekeza marekebisho kadhaa. Baadhi ya marekebisho hayo ni marekebisho ya kisarufi ambayo yana lengo la kuweka bayana matumizi sahihi ya maneno ili kuleta maana halisi iliyokusidiwa. Baadhi ya vifungu hivyo ni kifungu cha 55(1) cha Mswada ambapo neno "zitakazotungwa" lililopo baina ya neno "zozote" na neno "chini" linapendekezwa lisomeke "zilizotungwa". Aidha katika kifungu cha 47 cha mswada maneno ya pembeni ya kifungu hiki, yanapendekezwa yasomeke "Ritani na malipo".

Mhe. Mwenyekiti, kamati ya ngu pia, ilipendekeza kufutwa kwa baadhi ya vifungu vya Mswada huo kwa kuwa vifungu hivyo vilionekana havina msingi wowote. Baadhi ya vifungu vyenyewe ni kifungu cha 35(4) cha mswada ambacho kimejirejea tena kutokana na kuwa sawa sawa na kifungu cha 35(1).

Mhe. Mwenyekiti, marekebisho mengine yaliyopendekezwa na Kamati yangu ni kuweka usawa wa maneno baina ya Mswada wa Kiswahili na Mswada wa Kiingereza, ili miswada hii iendane. Mfano wa vifungu vilivyobainika kuwa na marekebisho hayo ni kifungu cha 51 cha mswada ambapo maneno ya pembeni ya kifungu hicho yanarekebishwa na kusomeka "Kamishna kutoa maoni". Aidha, Katika kifungu cha 71(a) cha Mswada neno "kuondosha" lililopo baina ya neno "au" na neno "stempu" linafutwa na kuweka badala yake neno "kuharibu".

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, kamati yangu imependekeza kuandikwa upya baadhi ya vifungu kwa kuwa mpangilio wake unaleta utata kwa msomaji. Mfano wa vifungu hivyo ni kifungu cha 73 cha mswada ambacho kinafanyiwa marekebisho kwa kuandikwa tena upya na kusomeka kama ifuatavyo:

"Mtu yeyote aliyeidhinishwa kuuza au kusambaza stempu, mtu huyo akiwa amekutwa na stempu iliyoghushiwa, hadi itakapothibitika vyenginevyo, itachukuliwa kuwa amekutwa na stempu, akijua kuwa imeghushiwa na amekusudia kuuza, kutumia au kuisambaza, atakua ametenda kosa na atatozwa faini isiyopungua shilingi laki tano 500,000 na isiyozidi shilingi milioni tano 500,000,000."

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu pia, ilifanya marekebisho kwa upande wa makosa ya kiuchapaji kwa lengo la kuweka bayana maneno yaliyotumika. Baadhi ya vifungu ambayo vilikuwa na makosa ya kiuchapaji na kufanyiwa marekebisho na kamati yangu ni pamoja na kifungu cha 2 cha mswada, ukurasa wa 61 kwenye tafsiri ya neno "hati ya kutokuwa na pingamizi": neno "kuthibisha" lililopo baina ya neno "hii" na neno "thamani" linapendekezwa lisomeka "kuthibitisha". Aidha, kwenye tafsiri ya neno "Kinachopaswa kutozwa": neno "kutumiaka" lililopo baina ya neno "kuanzia" na neno "kwa" linapendekezwa lisomeke "kutumika".

Mhe. Mwenyekiti, haya ni baadhi tu ya marekebisho yaliyopendekezwa na kamati yangu, marekebisho ya ziada yapo kwenye waraka wa kamati wa Mapendekezo ya Marekebisho ya Mswada huu, ambao natumai wajumbe wamepatiwa.

Hitimisho

Mhe. Mwenyekiti, naomba kukushukuru tena wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Bajeti. Aidha, naomba pia kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa kunisikiliza kwa utulivu kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako waujadili mswada uliopo mbele yetu, na hatimae waupitishe mswada huu muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kuwasilisha, ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Simai Mohamed Said wa Jimbo la Tunguu kwa uwasilishaji wako kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea na mchangiaji wetu wa mwanzo mpaka sasa niliyempata ni Mhe. Omar Seif Abeid. Lakini kabla ya kuendelea Waheshimiwa Wajumbe hii Miswada inahitajika tuipitishe leo na nahisi Waheshimiwa wengi sasa hivi wanaondoka wengine wanakwenda mazikoni, kwa hivyo nilikuwa naomba sana Waheshimiwa tuone kwamba huu Mswada wetu na tunahitaji sisi kuupitisha kama *quorum* basi nina imani huu Mswada utakuwa hatutautendea haki naaomba sana Waheshimiwa Wajumbe. Mhe. Omar Seif Abeid mchangiaji wa mwanzo na mpaka sasa hivi jina lako tu ndio liko hapa mezani.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kidogo nitoe mchango wangu wa mawazo kwenye Mswada huu ambao umewasilishwa leo hapa kwa dharura Mswada wa Sheria wa kuweka Masharti Bora ya Usimamizi wa Ushuru wa Stempu, mimi sina mengi nina mambo kidogo tu ambayo ningependa niyazungumzie.

Moja katika hili ilikuwa kwenye ukurasa wa 61 kwenye ufafanuzi kifungu cha pili juu pale unasema hati ya malipo naomba ninukuu "Itajumuisha hawala agizo la malipo" sasa nilikuwa nikitaka kidogo nipate ufafanuzi wa hili agizo la malipo kwa sababu kuna maagizo aina nyingi na niliomba kwanza Serikali ijue kwamba kuna biashara zinafanyika bila ya kupatikana kodi ya Serikali. Sasa nilitaka tupate ufafanuzi wa haya maagizo ya malipo kwa sababu mfano Mhe.

Mwenyekiti, tumezoea sasa hivi maagizo ya malipo mengi kwa wafanyabiashara wanaambiana tu mlipe huyo milioni ishirini yule anayepeleka malipo yale anakatwa ina maana pale biashara inafanyika, lakini idadi ile au faida ile haipati kuingia serikalini sasa nilitaka hili agizo la malipo nalo lifanyiwe ufafanuzi mkubwa ikijumlisha aina zote za biashara zitakazofanyika pale, nalo kwenye huo ufafanuzi lielezwe.

Lakini pia nikienda katika Ibara ya kifungu cha tatu hicho ukurasa wa 65 napenda kunukuu kifungu cha (a) katika usambazaji wa bidhaa na huduma Zanzibar mlipa kodi kutokana na uendeshaji wa biashara unaofanywa na mlipo kodi, usambazaji wa bidhaa ningependa kujua ni msambazaji wa aina gani aliyekusudiwa hapa. Kwa sababu wasambazaji wa bidhaa kwa sasa hivi tunaona na tumeshuhudia baada ya mzigo kuingia kutoka nje watu wanalipa ushuru bandarini wana *TRA*, wanalipa *ZRB* kla kitu wanafanya, lakini badala yake hawa hawana maduka, nilitaka nijue ni utaratibu gani utakaotumika na hii sheria nilipenda pia hapa vifungu hivi viweke wazi. Kuna watu hawana maduka wanachukua mizigo tu wanaweka stoo jambo hili pia linashusha si mapato tu linapunguza mapato, lakini linawaathiri wafanya biashara ambao ni walipa kodi halali.

Kwa hivyo nilikuwa nashauri hapa kwamba mtu yoyote anayeingiza mizigo kutoka nje awe ana duka au hana duka ambao wanasambaza mizigo yao au bidhaa zao waweze kutambulika na waweze kujulikana sehemu gani zinauzwa biashara hizo kisheria na ushuru wa serikali uweze kupatikana. Kwa hivyo hapa nilipenda katika kifungu hiki cha (a) kiwe na ufafanuzi wa kina, katika ufafanuzi huo uwaingize na hawa wasambazaji wa aina kama hiyo niliyowazungumza kwa sababu kama nilivyozungumza kwamba si kwamba wanawapunguzia au wanawakosesha serikali tu mapato lakini pia ni *challenge* kubwa kwa wafanyabiashara ambao ni walipa kodi halali.

Sijui ule utaratibu wa serikali kwa wale ambao pia wanasambaza bidhaa hizi wasambazaji wadogo wadogo wale wanaofanya biashara ukipiga hesabu kwa mwaka kama hapa pengine wanafika hata hiyo milioni kumi na tano, lakini bado wanaitwa ni wafanyabiashara wadogo wadogo wa mitaani na sijui utaratibu gani ule wa kupata kodi kutoka kwa wale au ndio serikali tumeamua kuwasamehe moja kwa moja kama wajasiriamali, lakini hawa wanafanya biashara kubwa na viwango vyao pengine vinazidi. Sasa hiyo milioni kumi na tano au pengine wanafanya biashara zidi kulikoni hata wenye maduka ambao wanakata leseni na kulipa ushuru.

Lakini kwenye kifungu hicho hicho kifungu cha 3(3) chini hapo kinachozungumzia ushuru wa Stempu napenda kunukuu (a) anasema "Kwa madhumuni ya kifungu cha 3(2) kifungu kidogo (a) na (b) kwamba kutakuwa na kiwango cha asilimia 3 kitakachotozwa kwa mujibu wa thamani ya kodi. Sasa hapa ukiangalia kwenye hilo Jadweli No. 4 utakuta kwamba hichi kiwango cha asilimia 3 kitakachotozwa kwa mujibu wa thamani ya kodi kwa watu watakaopatiwa msamaha samahani kidogo Mhe. Mwenyekiti, niangalie tena kidogo.

Mimi kwa upande wa wale watu ambao serikali imeamua kuwapatia msamaha nilikuwa napendekeza kwamba misamaha yote ya kodi ambayo inapatikana kwa ile asilimia 2 iliyotajwa iwe ni kwa thamani ya bidhaa, uingizaji wa bidhaa pale itakuwa rahisi kwetu sisi kupata uhalisia kulikoni kwenye mauzo, kwa sababu kwenye mauzo wanaweza wakadanganya hata kama

tunawaongezea kiwango lakini tupate kwa thamani ya bidhaa inayoingizwa. Kwa sababu pale itakuwa tayari kule tunakotoka imeshafanyiwa *inspection* na *valuation* ambayo inaonesha thamani halisi ya bidhaa inayoingizwa, sasa tukisema kwenye mauzo hapa kwenye mauzo watu wanajaribu kudanganya uhalisia wenyewe haupatikani na wengine wanadanganya wanapewa msamaha, wananchi hawafaidiki na msamaha huo kama tulivyozungumza juzi kuhusiana na watu wanaopewa misamaha. Mimi naomba sana suala hili la kutoa misamaha ya kodi viwango vya kodi isipokuwa labda kwa taasisi za kidini na mashirika kwa kazi maalumu za serikali ndio viwekwe viwango vya asilimia 2 au asilimia 3.

Vyenginevyo lakini viwango vya msamaha wa kodi viongezeke kidogo kwa sababu tunaona wananchi wanalalamika kwamba hata hicho chakula kinachosamehewa kodi kinakuwa punguzo la bei kwa wananchi wetu halionekani. Kwa hivyo kwa hapa nilikuwa napendekeza kwamba kwa watu watakaopatiwa msamaha iwe kwa ajili kama hiyo.

Lakini pia ninikienda katika ushuru wa Stempu kifungu cha 60 Viwango vya kutoza kwa bidhaa za huduma nchini, viwango hivi mfumo wa malipo kwa mkupuo inajumuisha bidhaa na huduma zinazotozwa kodi utakaofanywa kwa msingi wa robo mwaka kwa mlipa kodi na pale ikaainishwa robo ya mwaka ni upi. Lakini kwa mfanyabiashara mimi napendekeza kwamba hata tungempangia mara tatu ingekuwa vizuri zaidi kwa mwaka tukampa mwezi wa nne, Mwezi wa Nane na Mwezi wa 12 kulikoni kufanya miezi mitatu. Kwa sababu hapa nimeona tarehe 31 Machi, lakini mimi napendekeza ingelikuwa ni vipindi vitatu badala ya vipindi vinne kukawa na robo, nusu, kasorobo, asilimia 25, asilimia 50, asilimia 75 na *hundred percent*. Tungeifanya kwa asilimia kwa mara tatu pia ingekuwa ni vizuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa mswada huu na kwa sababu umekuja kwa dharura sina pingamizi nao na naunga mkono na nawaomba wenzangu wote tuunge mkono ili tuupitishe uweze kufanya kazi kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu sote kwa pamoja. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Omar Seif Abeid kwa mchango wako sasa naomba nimuite Mhe. Rashid Makame Shamsi.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi hii nikiwa mtu wa pili katika kuichangia au kuuchangia Mswada huu unaohusiana na Masharti Bora ya Usimamizi wa Ushuru wa Stempu, kwanza nimpongeze na nimshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kufikiria kuleta Mswada huu wa dharura katika Baraza hili, kwa lengo lile lile la kuhakikisha kwamba mapato ya nchi yanapanda siku hadi ili kuimarisha uchumi wetu.

Lakini vile vile nichukue fursa hii ya kuweza kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha kwa hotuba yake ya ufafanuzi juu ya malengo na umuhimu wa Mswada huu. Pia niwashukuru wenzetu wa kamati ya Bajeti kwa maelezo yao na nimpongeze sana Mhe. Simai Mohammed Said kwa uwasilishaji wake mzuri na ufasaha na umakini. Mswada huu ni Mswada ambao ni muhimu sana kama ulivyotangulia kusema kwa sababu unaweka utaratibu mzuri zaidi wa ukusanyaji na usimamizi wa ushuru wa stempu, lakini vile vile utakuwa unawapunguzia mzigo kama wenzetu walivyotangulia wale wafanyabiashara ndogo ndogo ambao walikuwa

wanalazimika kulipa ushuru mara mbili. Kwa hivyo hii itawapa faraja wafanya biashara wetu na hatimae kuwa na imani na Serikali yao na kuweza kufanya biashara ambayo itakuwa na tija na kuiletea Serikali mapato.

Mhe. Mwenyekiti, kwa tafsiri hiyo Mswada huu umekuja wakati muafaka utatusaidia na niwaombe sana ndugu wajumbe tuupitie na hatimae tuupitishe ili kuweza kuona kwamba nchi yetu inapiga hatua za kimaendeleo siku hadi siku, mimi nianze na masikitiko kidogo juu ya Mswada huu hususan kwa kamati ya bajeti au kwa utawala tunapokea marekebisho ya Mswada huu wakati hotuba inasomwa hii kwa kweli sio haki, unaleta mrekebisho hapa moto moto yanaunguza mikononi kwa kweli hatuwezi kutenda haki kama ni suala la Kamati ya Bajeti, kama nisuala la kiutawala lakini marekebisho yanayohusiana na Miswada tuyapate mapema kwa sababu sisi tuna kazi zetu tunachambua, sasa marekebisho yana page 31 katika kipindi hichi utapitia vipi lazima tufikirie hichi ni chombo tukufu hatuwezi kwenda hivyo. Lazima tuweze kufikiria kwamba hawa ni binaadam na wajumbe wanataka kuchambua. Sasa unapoleta marekebisho yana *page 30* wakati hati zishawasilishwa mezani na inasomwa nafikiri hilo hatuwezi kutenda haki.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije katika kuuchangia Mswada. Nije kwanza ukurasa wa mwanzo kwa hapa utakuwa ni ukurasa wa 60, ningeomba sana kwamba pamoja na kwamba Mswada huu unatokana na Mswada wa Kingereza majina haya ambayo yametolewa ufafanuzi yawekwe katika *Alphabetical* kabla haujaanza kutiwa saini.

Lakini nikija katika ukurasa wa 69 kifungu cha 12 (6)(b) kulikuwa na maneno pale, ningependa yasomeke kwenye mstari wa pili, palikuwa na maneno yameanza "yoyote meshindwa", basi naomba isomeke, "ameshindwa" na kuna neno "meshindwa", kuweka maelezo hapo maelezo yasomeke maelezo kamili na sahihi. Hayo maelezo yaliopo yaondoke kwa sababu neno la Kiingereza lililopo katika ule Mswada wa Kiingereza unasema, " *fails to fully and truly*", kwa hivyo yasomeke hivyo maelezo kamili na sahihi.

Lakini nikija katika ukurasa wa 70 Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 14 kuna maneno kwenye mstari wa nne, "herufi za mwanzo za jina hilo", kwa tafsiri ya *initial letters.* Mimi ningependekeza neno hilo lisomeke, "herufi za utambulisho", baada ya herufi za mwanzo za jina hilo", isomeke kwamba ni "herufi za utambulisho za jina la mteja" kwa lengo au kwa muktadha wa *initial letters*.

Lakini tukija katika ukurasa wa 73 Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 21 ukitizama Mswada ule wa Kiingereza kifungu cha 21 ule wa kiingereza una vifungu vitatu (a), (b) na (c), lakini kwa bahati mbaya katika huu wa Kiswahili kifungu kile kimekuwa kimerukwa hakipo. Kwa hivyo ningeomba hicho kifungu kiingizwe ambacho katika Mswada wa Kiingereza kilianza na neno, "*Where the sum is payable for an indefinite.* Hilo neno au hicho kifungu itabidi kitafsiriwe halafu kije kiingizwe hapa.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika ukurasa wa 78 vile vile kuna kifungu ambacho kimerukwa ambacho kilikuwa ni kifungu cha 7, huo ukurasa umeanza na kifungu cha 4,5,6, kifungu cha 7

hakipo ambacho katika *version* ya Kingereza kifungu hicho kipo ambacho kimeanza na *where any person.* Kwa hivyo ningependa kitafsiriwe halafu kiingizwe hapo.

Lakini tukija katika ukurasa wa 79 kifungu nambari 6, kwanza kuna kifungu cha 5 kimeanza ukurasa wa 78 kimemalizia ukurasa wa 79 kwa vifungu vidogo (a) na (b). Sasa hapo ilitakiwa kiwepo na kifungu nambari 6 ambacho katika Mswada ule ulioandikwa kwa lugha ya Kingereza basi kipo ambacho kimeanza na neno, *"For the purpose of this* act...."*.*

Mhe. Mwenyekiti, nielekee sasa katika ukurasa wa 80 kwenye kifungu cha 40 maneno yanayomalizia pale, "kwa asilimia ya dhamana hiyo". Katika maelezo ya Kingereza kuna maneno "*on the value of such security"*. Kwa tafsiri hiyo muktadha huo utakuwa umekosekana. Nilikuwa napendekeza isomeke, "kwa thamani ya dhamana hiyo".

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 81 katika kifungu cha 44 kwenye neno la pembeni hapo ambalo linasema "Mfanyakazi wa Benki au Hawala ya Benki". Katika Kingereza hakuna neno "au", lipo neno "na", yaani "and". Kwa hivyo lisomeke vile vile "mfanyakazi wa Benki na Hawala ya Benki."

Lakini vile vile katika kifungu hicho hicho mstari wa pili ambao umeanza na shughuli za kibenki Zanzibar zenye uhusiano na Benki. Sasa hapo uhusiano na Benki, hilo neno napendekeza liondoke, katika *version* ya Kingereza kuna neno *banker,* kwa maana ya mfanyakazi wa benki. Kwa hivyo lisomeke kwamba, "zenye uhusiano na mfanyakazi wa benki na hawala za benki", na sio uhusiano na benki.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika ukurasa wa 83 kifungu cha 50 neno la pembeni ambalo ni "hati ambazo hazijawekwa stempu hazitotumika kwa ushahidi". Ningependa hilo neno lisomeke "halitotumika katika ushahidi", *in evidence.*

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 87 kuna vifungu vidogo hapo kifungu kidogo cha (c) ambacho kina vifungu vitatu. Kifungu cha 3 kimeandikwa kifungu cha 2, kwa hivyo irekebishwe iwe kifungu namba 3.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 88 kifungu cha 59(2) pana aya ambayo imesemwa hapo ina mistari kama 7, lakini kuanzia mstari wa nne unaosomeka, "hadi nakala iliyochapishwa". Maelezo haya ni maelezo ya ziada ambayo hayamo kabisa katika *subsection* ile ya Kingereza. Sasa sijui muktadha utakaaje kwa sababu ni maelezo mengi sana ambayo yamejazwa hapo, sijui yamepatikana wapi au labda Mwanasheria aje atuwekee sawa kwa nini yakaingia maelezo karibu mistari mitano ambayo kwenye *version* ya Kingereza hayo maelezo hayapo.

Mhe. Mwenyekiti, nije ukurasa wa 89 katika nembo iliyopo juu Sehemu ya Nne, "ushuru wa stempu katika biashara". Hapo naona pawe na neno "katika kuendesha biashara", nafikiri ndivyo ambalo lilipaswa liwe hivyo, "Ushuru wa stempu katika kuendesha biashara", lisomeke hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile katika kifungu cha 60 neno la pembeni, "viwango vya kutoza" kwa muktadha lisomeke, "viwango vya tozo". Lakini tukija katika kifungu hicho hicho cha 60(2) ambacho kina vifungu (a), (b) na (c) katika *version* ya Kingereza. Katika *version* ya Kiswahili kifungu hichi cha (c) kimejumuishwa na kifungu cha (b) ambacho kinaanzia hapo katika mstari wa pili neno la mwisho penye neno "kuongeza", hapo ndiyo palipaswa paanzie kifungu cha (c) ukiangalia *version* ya Kiingereza. Kwa hivyo hicho kishuke kiweze kuweka vifungu vitatu kama ilivyo kwenye *version* ya Kingereza.

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa katika ukurasa wa 90 wa Mswada huu kwenye kifungu ambacho kipo juu hapo, kifungu hicho herufi iliyowekwa ni herufi (a) lakini isomeke kwamba ni herufi (c). Lakini hata katika muktadha kwamba, "shughuli zinazofanywa na taasisi za serikali". Hayo maneno napenda yarekebishwe yawe ni, "shughuli inayofanywa na taasisi ya serikali", kutokana na maelezo yaliyokuwepo katika *version* ya Kingereza, ametumia neno, "*activity",* na sio "*activities"*. Kwa hivyo kunapaswa kuwa na marekebisho katika hilo.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije kwenye ukurasa wa 95 kwenye kifungu cha 77(2) ambapo imeeleza kwamba mstari wa pili, "ushuru hautatozwa katika nyaraka zifuatazo". Neno lilotumika kule ndilo ambalo tunaliamini katika ufafanuzi wa maneno ni, "neno hati", yaani *instrument.* Kwa hivyo hilo "nyaraka", ningependa liondoke na likae neno "hati", kama neno ambalo limeelezwa katika ufafanuzi wa maneno ya mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti, ukija kifungu cha 78(1)(b) kuna neno limeanza na "namana". Ninapenda lisomeke, "namna", ndivyo ambavyo linaleta muktadha mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie sasa katika ukurasa wa 96(3) ambacho kinaonyesha kwamba, "Jambo lolote lililofanywa chini ya sheria iliyofutwa, litachukuliwa kama limefanywa chini ya sheria hii".

Mhe. Mwenyekiti, hapa kidogo nina wasi wasi, naomba Mwanasheria atakapokuja aweze kutuweka sawa. Hii sheria tunaifuta, maana yake tunaunda Sheria mpya ambayo ndiyo hii ambayo hivi sasa tunaijadili. Mhe. Mwenyekiti, sasa unaposema kwamba jambo lolote lililofanywa chini ya Sheria iliyofutwa, litachukuliwa kama limefanywa chini ya Sheria hii, kidogo kuna utata. Kwa sababu Sheria iliyofutwa ndiyo imefutwa na kama kulikuwa kuna Kanuni zake zote zitakuwa hivi sasa hazitofanya kazi kwa sababu ya kupitisha Sheria hii mpya. Sasa unaposema kwamba litachukuliwa kama limefanywa chini ya sheria hii mimi kidogo nina utata ingawa si mwanasheria, lakini Mwanasheria anaweza kuja kutuweka sawa, ili kuja kuondosha mgogoro. Kwa sababu mtu anaweza kuwa kafanya jambo kule lakini kwa mujibu wa sheria, hivi vifungu vilivyobadilishwa ikawa ukaja ukakuta kwamba pengine hana hatia.

Ningependa Mwanasheria aweze kulitizama vizuri hili ili lisije likaleta utata baadae kwa sababu kuna makosa au kuna mambo ambayo yamefanyika huko nyuma kwa sheria ambayo tunaifuta, halafu mtu pengine tunaweza tukaja tukamuadhibu kwa sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa nafasi hii ambayo umenipa na niwaombe sana wenzengu waupitie Mswada huu na kuweza kuchangia. Mimi ninaunga mkono kwa asilimia mia

kwa mia Mswada huu ili serikali iweze kukusanya mapato zaidi na kuwaondoshea mzigo wafanyabiashara wa kulipa ushuru mara mbili.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Rashid Makame Shamsi kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Shehe Hamad Mattar.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Asante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii niweze kutoa machache katika mchango wangu kwenye Mswada uliyokuwepo mbele yetu. Kwanza sina budi nikupongeze sana wewe Mwenyekiti, lakini pia pongezi zaidi ziende kwa serikali kwa kuona kwamba kile kilio cha wananchi wetu kimesikika.

Serikali imekuwa siku zote ikipokea malalamiko kwa kuona kwamba wananchi wanapiga kelele kwamba tunalipa kodi mara mbili, kwa hivyo bidhaa zinakuwa ni ghali kutokana na kwamba kila pahali tunalipa kodi. Lakini leo serikali imeliona hili kwamba lilete turekebishe sheria hii na kuona kwamba unafuu wa wananchi wetu unapatikana na wao wawe na hamu ya kuweza kulipa kodi bila ya kushurutishwa. Pia nimpongeze sana Mhe. Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuleta Mswada huu kwa Dharura na kwa haraka sana ili uweze kufanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu mimi ni mchache sana kwa sababu ni Mjumbe wa Kamati lakini niiyombe serikali kwamba hapa tunakuwa tunapitisha sheria hapa mbali mbali ambazo tumetunga na nyengine walizozitunga wenzetu. Lakini inakuja kuwa na utata kwamba sheria ile baada ya kutungwa inabaki ndani ya vitabu haitekelezwi, kwa mwananchi anabaki kufanya anavyotaka na siku ambayo kuwa utaanza kuichukulia hatua sheria ifanye kazi ukafungue kitabu anakwambia sheria hiyo mimi siitambui wala haijulikani. Kwa mujibu wa sheria haijui kwamba wewe unajua wala haijui kama ipo na kama umeivunja ndiyo unaweza kutiwa hatiani.

Naiomba sana serikali kwa zile taasisi zitakazokuwa zinasimamia utekelezaji wa sheria hii wawe makini sana na kuona kwamba sheria zetu zinazopita hapa zinathamani. Muda tunaoutumia hapa ni mwingi, akili tunayotumia hapa ni nyingi, fedha tunazotumia hapa ni nyingi kwa hivyo kile tunachokitunga hapa kiweze kuleta tija katika nchi yetu. Ni dhahiri kwamba sasa wananchi wataona kwamba serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi inavyoendelea kuwajali, kilio chao kimesikika na leo ndiyo hapa tunapitisha sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, niwaombe wale watakaokuwa watekelezaji wa sheria hii na wao wawe waaminifu kwao wao wenyewe na wawe waaminifu kwa serikali yao ambayo kuwa inatuongoza ikisimamiwa na Chama cha Mapinduzi. Leo tunaweza tukaondoa ushuru kama huo kwa kuweka unafuu kwa mfanyabiashara lakini pia unafuu kwa mwananchi hatimaye kile kitu tunachokiondoa kinabaki kwenye mifuko ya wale wanaokuwa wanasimamia sheria hii. Wameondoka kwenda kufanya kazi kwa niaba ya serikali lakini hatimaye huwa wanatunisha mifuko yao. Hapa ndiyo tunapokuja kupata ugumu wa kwamba tunatunga sheria lakini kumbe tunamfanyia mtu manufaa yake yeye badala ya wananchi waliyowengi.

Niiyombe sana serikali hapa tuwe wakali katika kusimamia suala hili. Kwa mfano serikali sasa hivi imeondoa ushuru wa bidhaa ambazo kuwa ni muhimu kwa mwezi wa Ramadhani kwa lengo la kumsaidia mkulima na mfanyakazi lakini leo unakuta bidhaa zimepanda haraka kama ilivyokuwa haikutaka serikali kabisa. Serikali imeondoa ushuru na kwa sababu wananchi wapate unafuu hasa mwezi huu wa Ramadhani lakini hatimaye ndiyo wafanyabiashara wamefungashia kuona kwamba hii ndoma hivi sasa ndiyo hapa pa kupatiza. Hili jambo mimi binafsi nalilani sana na hawakulifanyia wema serikali yao ambayo kuwa imewaondolea ushuru ule.

Na hili tunaondoa ushuru wa kulipa kodi mara mbili na pia ushuru wenyewe umepunguza, ukitizama viwango vingi vimepunguzwa kwa bidhaa na huduma zinazotolewa nchini zimepunguzwa kulingana na ilivyokuwa zamani. Lakini sasa isijeikawa anataka mchanga, anataka bidhaa yoyote ile nondo anakwambia ushuru umepanda hicho kitu hakuna. Nawaomba wananchi waelewe kwamba hakuna kodi iliyoongezwa bali kuna kodi iliyopunguzwa. Kodi imepunguzwa kwa kuwasaidia wananchi wake waendelee kufurahia Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi naomba sana kwamba serikali ikifanya hivi ndiyo tutaweza kuendelea na tutaendelea kushinda mwaka 2020 bila ya matatizo yoyote. Kwa sababu tayari tunawajali wananchi na itakuwa ni tofauti na wale ambaokuwa wanajidai wanawajali wananchi wao lakini siyo kweli.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na kutunga sheria hii namuomba sana Mwanasheria Mkuu na yeye anahusika kutunga na Kanuni kwa sababu sheria inaweza ikatiwa saini leo hapa lakini ukasikia haijaundiwa Kanuni kwa hivyo haiwezi kutekelezeka. Naomba sana Kanuni nayo iende haraka sana iwezekanavyo ili sheria iweze kutekelezeka.

Baada ya hayo niseme naunga mkono Mswada huu mia juu ya mia naomba sana tuwe watekelezaji wakweli tusibaki kwenye vitabu tu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Shehe Hamad Mattar kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajume huyo ndie alikuwa ndiyo mchangiaji wetu wa mwisho sasa naomba nimwite Mhe. Waziri ili atoe ufafanuzi juu ya yale masuala yaliyojitokeza. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango karibu.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kutoa shukurani za dhati kabisa kwa Waheshimiwa Wajumbe wale waliopata fursa ya kuchangia lakini hata wale waliokuwa hawakupata fursa ya kuchangia. Naamini waliokuwa hawakupata fursa ya kuchangia wameunga mkono hoja yangu. Kwa sababu tulipata muda mzuri sana wa kuijadili Miswada ya Sheria hiyo wakati tulipofanya semina, naamini imesaidia.

Pia nichukue fursa hii Mhe. Mwenyekiti, kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati na Makatibu wa Kamati kwa sababu wamefanya kazi kubwa sana na nzuri sana baada ya Mswada wa Sheria hii kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu waliupitia kwa kina, walipitia kifungu kwa kifungu na walifanya marekebisho mengi yaliyostahili na waliyoweza kuyaona.

Nimshukuru sana Mhe. Simai Mohamed Said Mwakilishi wa jimbo la Tunguu, kwa kutoa taarifa ya Kamati ya Bajeti na kuainisha maeneo ambayo wameendelea kuhisi kwamba kuna haja ya kuangalia kwa umakini zaidi kwenye Mswada wa sheria hii.

Lakini vile vile nimshukuru sana Mhe. Omar Seif Abeid kwa michango na maoni yake aliyoyatoa. Nimshukuru sana sana Mhe. Rashid Makame Shamsi inadhihirisha kabisa kama kawaida yake Mhe. Rashid Makame Shamsi ameupitia kwa kina kabisa. Mengi aliyoyaona ni kweli na mengi yao yalionekana na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Bajeti walipokuwa wakipitia rasimu hii. Kwa hiyo yapo ambayo tayari yameshafanyiwa marekebisho na Kamati ya Bajeti lakini na yako mapya ambayo nimueleze tu kwamba tuna *appreciate* sana kwa *observation* yake ya tunayachukua. Lakini pia nimshukuru sana Mhe. Shehe Hamad Mattar na yeye ni mjumbe wa Kamati lakini pia amekuwa na maoni ya ziara, namshukuru sana kwa hilo na nitatoa ufafanuzi baadaye kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye michango iliyotolewa na Kamati ya bajeti Mheshimiwa niombe nieleze mambo machache ni kwamba Mswada huu kwa kiasi kikubwa sana na tumejitahidi sana na serikali imejitahidi sana kuweka unafuu mkubwa sana kwa walipa kodi wadogo. Kama alivyosema Mhe. Shehe Hamad Mattar kwamba viwango vimepunguzwa na vimepunguzwa sana hata ukitizama viwango vilivyowekwa katika sheria ambayo tunapendekezwa ufutwe Sheria ya Ushuru wa Stempu ya mwaka 1996 na hii ya sasa hivi. Utakuta kwamba viwango vingi vimepunguzwa na ni vidogo sana.

Lakini pia kumewekwa utaratibu utakaotoa unafuu wa walipa kodi wenyewe, kwa maana sasa walipa kodi hasa walipakodi wadogo hawatotakiwa kulipa katika vyombo viwili kwa maana ya *TRA* na *ZRB* watatakiwa walipe *ZRB* peke yake, nao huo ni unafuu mkubwa sana. Ukitizama hata viwango walivyokuwa wakilipa kwa kupitia sheria iliyokuwepo sasa ambayo inafutwa. Viwango walivyokuwa wakilipa *TRA* na *ZRB* ukivijumlisha pamoja na hivyo watakavyolipa sasa hivi, hivi viko chini sana. Kwa hivyo imewekwa makusudi na serikali imeweka hivyo kwa sababu ya kukuza fursa ya biashara katika nchi yetu lakini vile vile kukuza fursa ya ajira kwa watu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Omar Seif Abeid katika kifungu cha 3(2)(a) aliliulizia kwamba usambazaji wa bidhaa huo ni usambazaji wa aina gani, alitaka ufafanuzi kwenye maeneo hayo.

Niseme tu kwenye kifungu cha 3 kinaweka utaratibu mzima wa utozaji wa kodi hii na pale kuna wale wasambazaji waliotajwa katika kifungu cha 3(2)(a) na hawa wanahusishwa wale wote wasambazaji ambao wanafanya biashara zao nchini ndiyo wanaokusudiwa katika kifungu hichi. Hii haihusishi mizigo inayotoka nje ya nchi, mizigo inayotoka nje ya nchi inahusisha siyo sheria hii, lakini ziko na sheria nyengine ambazo zinahusika ikiwemo Sheria ya *VAT* ya mwaka 1998. Hii inahusu usambazaji wa bidhaa na huduma kwa wafanyanyabiashara waliokuwepo nchini na haihusiani na mizigo inayotoka nje.

Mhe. Mwenyekiti, nimueleze kwamba asiwe na wasi wasi *ZRB* itafuatilia kwa makini sana bidhaa zilizokuwepo kwenye magodauni, zilizopo kwenye maghala na kuhakikisha kwamba *VAT* inalipa kwa ukamilifu wake. Kwa hiyo kazi hiyo itafanyika na asiwe na wasi wasi lakini

hata ukitizama sheria tuliyonayo Sheria ya Usimamizi wa Kodi (*Tax administration Procedures Act)* nayo imeweka utaratibu maalum wa usajili wa maghala kwa hivyo ipo sheria inayohusika na hilo na kazi hiyo itafanyika.

Lakini ndani ya kifungu hiki cha tatu kimeweka utaratibu wa *code* zile ambazo zinastahiki kutolewa kwa wafanyabiashara waliosamehewa kulipa kodi ya *VAT* na kwa biashara maalum kwa mfano mchele umesamehewa kodi ya *VAT*, lakini vile vile unga wa ngano umesamehewa kodi ya *VAT* sasa watalipa chini ya utaratibu wa kifungu hiki cha sheria na watalipwa imeelezwa watalipwa asilimia mbili (2%) ya thamani ya mzigo wote.

Lakini pia kuna katika kifungu hiki kimeweka utaratibu wa zile hati na mara hii katika sheria mpya tunayoipendekeza zile hati zote zimeaninishwa ambazo zitapaswa kulipiwa ushuru wa stempu, zimeanishwa vizuri na zimewekwa vizuri na viwango vyao kuwekwa vizuri katika jadweli na kuhakikishwa kwamba viwango hivyo vimepunguzwa ili kutoa unafuu.

Lakini pia sheria hii mapendekezo ya sheria hii yameweka utaratibu kwa walipa kodi wadogo wadogo na upo utaratibu mzuri ambao umeelezewa katika kifungu cha 60 ya kulipa kodi kwa mkupuo, kwamba kila robo mwaka wanatatakiwa walipe. Lakini hata hivyo mtu akitaka kulipa kiwango kikubwa zaidi au alipe mwanzo basi hakatazwi anaruhusiwa na sheria inamruhusu kufanya hivyo, lakini hii tuliweka kwa unafuu walipe kila robo mwaka kwa hiyo nawashukuru sana kwa mchango huo.

Nileze tu kwamba hati za malipo ambazo ni *instrument* kama nilivyosema zimeweka katika kuhakikisha kwamba miamala ya fedha yote inayofanyika kwa mujibu wa sheria hii basi inalipiwa kodi zinastahiki, na kuna swala zima ambalo litawekwa ndani ya utaratibu wa kanuni imeelezwa na Mhe. Shehe Hamad Mattar kwamba tuharakishe kuhakikisha kwamba kanuni zinawekwa, nimuhakikishe tu kwamba sheria hizi zinahitaji kutekelezwa katika utekelezaji wa bajeti ambayo tumeshaipitisha ya mwaka 2017/2018 na ndio maana inaletwa hii kwa hati ya dharura kwa sababu inatakiwa kwamba iwe ni *instrument* ya kutekeleza bajeti yetu ambayo tumeipitisha. Kwa hivyo suala la kanuni suala hilo wasiwe na wasiwasi sisi tumejipanga na kanuni hizo zitatayarishwa kwa haraka sana ili mswada wa sheria hii utakapopitishwa uweze kutekelezwa.

Kuna suala lilizungumzwa la misamaha nalizungumzia suala la misamaha ya asilimia mbili (2%) kutowela misamaha ya asilimia mbili (2%) na hili niseme kwamba misamaha ya asilimia mbili (2%) kutolewa kwa kuzingatia thamani ya bidhaa wakati inapoingizwa nchini, kwa zile bidhaa ambazo sasa hazitozwi kodi kwa kusamehewa kupitia sheria ya *VAT* ambayo sasa zitatakiwa zilipe asilimia mbili (2%) kwa hivyo, punguzo au kusamehewa kulipa kodi hiyo kunatokana wakati mizigo hiyo inapoingia nchini. Kwa sasa bidhaa za mchele na unga kama nilivyosema zinatozwa asilimia mbili (2%) na fedha zinalipwa wakati bidhaa hizo zinapoingizwa nchini.

Serikali niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba itandelea kufatilia ili wafanya biashara wanaopata misamaha hii waweze kuitumia vizuri misamaha hii, bila ya shaka kwa faida yao lakini vile vile kwa manufaa mapata zaidi na manufaaa makubwa ya wananchi wetu. Kuna hii ya kifungu cha 60 kilichozungumzwa tayari nimeshakieleza kwamba kinatoa unafuu mkubwa

sana kwa kulipa kodi ya mkupuo kwa maana mara nne vipindi vinne kila robo mwaka lakini mtu hatozuiwa sheria haizuii wala haipingi, sheria hii inayopendekezwa ya stempu wala sheria ya TAPA haizuwii wala kupinga mtu kulipa mapema zaidi na kwa mujibu wa kifungu cha 32 cha Sheria TAPA kinaruhusu *early payment* atangulize malipo.

Mhe. Shamsi yeye alizungumzia zaidi katika masuala ya *typelogical,* na ameainisha kama nilivyosema mwanzo inaonesha wazi kwamba ameusoma vizuri amegundua mambo mengi na nimwambie tu yote tunayapokea, lakini miongoni mwa hayo mengi yameshafanyiwa kazi na kamati. Kwa mfano liko hili la kifungu cha 14(1) suala lililoeleza harufi za mwanzo za jina iwe herufi tunalichukuwa na pia alilizungumzia suala la hati hazitatumika katika ushahidi, nalo tunalichukuwa lakini pia alizungumzia suala la kifungu cha 12(6)(b) maelezo yote ni maelezo kamili na sahihi na hilo Mhe. Mwenyekiti tunalichukua na tutalifanyia kazi lakini sambamba na yale yote yaliyogunduliwa na Kamati ambayo tayari wameshayatolea maelezo yake.

Kuna suala jengine alilizungumza Mhe. Rashid Makame Shamsi ya kifungu cha 79(3) alizungumzia kwamba sheria hii ile sheria inayofutwa sasa yale mambo yaliyotendeka wakati huo sheria ile ikitumika yatabakizwa na sheria hii. Nimweleze tu na nafikiri Mwanasheria Mkuu atakubaliana na mimi kwamba sheria zote zinazotungwa huwa kuna kifungu kinachobaliza, kwa maana *services* na hiki kinawekwa makusudi kwa mtizamo wa kisheria kwamba kusiweko na *vacuum* baina ya Sheria ile inayofutwa na Sheria hii mpya itakapoanza kutekelezwa. Hilo moja.

Lakini la pili kuna mambo ambayo yamekwisha tendeka kwenye hiyo inayofutwa sasa lazima yabakizwe na sheria hii ili yaendelezwe yaendelee kubaki kuwa halali, vyenginevyo kama mtu ulimtonza kodi kwa sheria ya mwaka 1996 kwa kiwango cha juu na sheria ya sasa inafuta inapunguza kwa kiwango cha chini, bila ya kubakiza yale matendo yaliyofanywa kule ile mtu anaweza kuja kukudai kodi yake akasema kwa mujibu wa sheria ya sasa mlinitonza kubwa zaidi kwa hivyo nilipeni fedha ambayo nililipa ya ziada. Sasa hii inawambia yale matendo bado yanabaki kuwa halali kwa hivyo hatakuwa na haki ya kudai kile alicholipa wakati yule, kwa hichi mtegemee kwa makusudi hayo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Shehe Hamad Mattar yeye alizungumzia suala la uaminifu watendaji, uadilifu wa watendaji na nimuhakikishe kwamba hili ndio suala ambalo tunalipigia kelele sana kuhakikisha kwamba sote watendaji, viongozi tunaosimamia maswala ya mapato ya Serikali tunafanya kazi hiyo kwa uadilifu mkubwa ili kuwasaidia wananchi wetu na kuiletea maendeleo nchi yetu, asiwe na wasiwasi na hilo na kanuni kama nilivyomueleza tunazifanyika kazi kwa haraka sana ili sheria hii iweze kutekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema haya nirudie kuwashukuru wale wote waliochangia, niwashukuru wote waliosaidia kwa namna moja au nyengine kuwandaa mswada wa sheria hii.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa naomba niwahoji wanaoafiki wanyooshe mikono na wanaokataa hoja hiyo, wanaoafiki wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria, ili kuupitia mswada huu kifungu kwa kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Ushuru wa Stempu ya Mwaka 2017

Sehemu ya Kwanza

Utangulizi

Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika
Kifungu 2 Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Pili

Utozaji Kodi na Utawala

Kifungu 3 Pamoja na marekebisho yake
Kifungu 4 Hati ya kutokuwa na pingamizi pamoja na marekebisho yake
Kifungu 5 Utawala pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Tatu

Masharti ya Jumla Yanayohusika na Hati

Kifungu 6 Hati zinazostahiki kutonzwa kodi pamoja marekebisho yake.
Kifungu 7 Mtu anayewajibika kulipia pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 8 Utambuzi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 9 Namna hati zinavyoandikwa na kuwekwa stempu pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 10 Adhabu kuhusiana na stempu ya wazi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 11 Uwekaji wa stempu kwa baadhi ya hati pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 12 Uchunguzi na uuziaji wa hati pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 13 Ufutwaji wa stempu pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 14 Ufutaji kwa mawakala walioteuliwa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 15 Thamani ya mali inayostahiki kulipiwa kodi.

Kifungu 16 Maelekezo kuhusiana na ushuru wa baadhi ya hati za uhaulishaji mali pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 17 Sehemu au upande.
Kifungu 18 Hati za uingizaji na usafirishaji wa bidhaa.
Kifungu 19 Hati ya malipo na hawala pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 20 Uhaulishaji kwa njia ya mauzo.
Kifungu 21 Tathmini ya malipo kwa vipindi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 22 Athari ya maelezo ya thamani.
Kifungu 23 Namna ya kuhesabu kiwango cha ushuru kwa asilimia pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 24 Uhaulishaji wa makubaliano ya deni au malipo ya baadae.
Kifungu 25 Rehani pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 26 Uhaulishaji wa hiari pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 27 Dhamana kwa malipo awali yatakavyotozwa ushuru pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 28 Namna ya ukodishaji kutozwa mrahaba pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 29 Ushuru wa ukodishaji kwa mazingira mengineyo pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 30 Namna ya kutoza ukodishaji katika uzalishaji au vyenginevyo pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 31 Ushuru katika ukodishaji wenye kodi tafauti pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 32 Hati hazitathibitishwa kwa kiapo mpaka ziwekwe stempu pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 33 Sera za bima pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 34 Sera za bima ya usafiri wa bahari pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 35 Mkataba wa ukodishaji chombo cha usafiri pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 36 Kuwekwa stempu makubaliano ya ukodishaji kwa madhumuni ya kununua pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 37 Utiaji thamani hisa na dhamana za soko pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 38 Uhaulishaji wa nyaraka za hisa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 39 Uhaulishaji kwa njia ya mauzo.
Kifungu 40 Usawizishaji wa deni pamoja na marekebisho yake.
KIfungu 41 Ikiwa hati mbali mbali moja tu inatozwa.
Kifungu 42 Dhamana za hisa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 43 Hundi zilizokuwa hazijawekwa stempu pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 44 Mfanyakazi wa benki au hawala ya benki pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 45 Masharti ya kutoza ushuru wa risiti pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 46 Utaratibu wa ushuru katika risiti pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 47 Marejesho na malipo pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 48 Hati zitakazotozwa ushuru tafauti pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 49 Kivuli na nakala pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 50 Hati ambazo hazijawekwa stempu hazitotumika kama ushahidi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 51 Maoni ya Kamishna pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 52 Uwezo wa Kamishna kurejesha malipo ya adhabu au ushuru uliozidi kwa baadhi ya mazingira pamoja na marekebisho yake.

Kifungu 53 Tathmini ya ushuru kwa mazingira maalumu pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 54 Muda wa kuweka stempu nyaraka pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 55 malipo kwa stempu zilizoharibika pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 56 Mazingira ya stempu zilizoharibika pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 57 Malipo katika kubadilisha stempu pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 58 Tathmini ya Mtathmini wa Serikali.
Kifungu 59 Kumbukumbu za kielotroniki pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Nne

Ushuru wa Stempu katika Biashara

Kifungu 60 Viwango vya kutoza pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 61 Shughuli zinazotozwa kodi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 62 Thamani inayotozwa kodi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 63 Utambulisho wa walipa kodi.
Kifungu 64 Udhibiti tathmini na ukusanyaji pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 65 Mfumo wa malipo ya ushuru pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 66 Marejesho na maelezo yake pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 67 Ukadiriaji wa thamani pamoja na marekebisho yake.

Sehemu ya Tano

Mengineyo

Kifungu 68 Kushindwa kuonesha maelezo sahihi kuhusiana na hati pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 69 Usajili wa hati zisizowekewa stempu sahihi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 70 Kuweka kikwazo katika usimamizi wa sheria hii pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 71 Makosa yanayohusiana kuweka stempu katika hati, kuondosha na ukwepaji wa ushuru pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 72 Kumiliki hati ambazo zimewekwa stempu kinyume na sheria pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 73 Stempu zilizoghushiwa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 74 Adhabu za jumla pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 75 Uwezo wa kuchunguza pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 76 Uwezo wa kupata taarifa pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 77 Uwezo wa kusamehe malipo ya ushuru katika hati pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 78 Kanuni pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 79 Kufuta na kubakiza pamoja na marekebisho yake.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kukubali pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa sasa naomba niwahoji waliokubali wanyanyue mikono, na wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Ushuru wa Stempu ya mwaka 2017

(Kusomwa kwa mara ya Tatu)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Ushuru wa Stempu ya mwaka 2017 usomwe kwa mara ya tatu.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa naomba niwahoji waliokubali wanyanyue mikono, na waliokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya Tatu na kupitishwa)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri na wajumbe wote waliochangia kwa mswada huu kwa kupitisha nina imani Mhe. Waziri utaufanyia kazi kama ipasavyo. Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea.

Mswada wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa na Huduma ya 2017

(Kusomwa kwa Mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, mswada ninaouwasilisha ni mswada unaowasilishwa kwa Hati ya Dharura, kwa hivyo naomba kusoma hati ya Mhe. Rais wa Zanzibar kama ilivyo na kwa mujibu wa Kanuni ya 80 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2016.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kusoma hati ya Mhe. Rais wa Zanzibar kama ilivyoandikwa.

Tangazo Nam. 48, Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2016. Shahada ya Mswada wa Sheria wa Dharura chini ya Kanuni ya 80 kwa uwezo niliopewa chini ya Kanuni ya 80 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2016, mimi Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi natamka kwamba Mswada wa Serikali wa Kuanzisha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa ni wa dharura na wa haraka sana, na kwamba haiwezekani kutimiza masharti ya Kanuni ya 79. Umetiwa saini na muhuri wa Rais tarehe 12 Mei, 2017 lipo jina la Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na saini yake.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba sasa kutoa hotuba yangu inayohusu mapendekezo ya Mswada wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria mpya ya Ushuru wa Bidhaa na sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mhe. Mwenyekiti, kama ilivyo desturi naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhana Wataalah kwa kutujaalia afya njema iliyotuwezesha kukutana katika Baraza hili kukamilisha shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika kikao hiki. Miongoni mwake ni kujadili Mswada wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa unaosomwa kwa mara ya pili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mara nyengine naomba kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa), nimshukuru pia Makamu wake Mhe. Bahati Khamis Kombo pamoja na Wajumbe na Makatibu wote wa Kamati kwa michango yao waliyoitoa wakati wa kupitia mswada huu. Pia niwashukuru watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango na taasisi za ukusanyaji ikiwemo Bodi ya Mapato (*ZRB*) na Mamlaka ya Mapato tawi la Zanzibar (*TRA*). Pia shukurani zangu za dhati kabisa nazitoa kwa wadau wote wa *Tax Reform Task Force* kwa michango yao waliyoitoa wakati wa matayarisho ya mswada huu ambao leo unasomwa kwa mara ya pili.

Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa jitihada zake na mashirikiano wanayotupatia wakati wa matayarisho ya miswada ya sheria zinazosimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango. Pia naomba niwashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa michango yao wanayoitoa kuimarisha miswada ya sheria ninayowasilisha katika kikao hiki.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijawasilisha madhumuni ya mswada naomba nieleze historia fupi inayohusiana na ushuru wa bidhaa.

Ushuru wa bidhaa aghlabu hutozwa kwa bidhaa ambazo ama matumizi yake yanachukuliwa kuwa ni anasa au yenye madhara kwa jamii. Dhamira ya ushuru huu kinadharia huwa zaidi ni kupunguza matumizi ya bidhaa hizo. Hata hivyo, kumejitokeza pia mazoea ya kutoza ushuru huo kwa dhamira ya kuongeza mapato ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, mtakumbuka kuwa kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki iliyohusisha nchi tatu za Kenya, Uganda na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1977 kulipelekea ushuru huu kukusanywa nchini kama jambo la Muungano. Kwa wakati huo ushuru ulikusanywa zaidi katika bidhaa zinazozalishwa nchini. Mwaka huo huo wa 1977 Jamhuri yetu ya Muungano pia ilipitisha Katiba yake ya kwanza ya kudumu na kuufanya ushuru huo wa bidhaa zinazozalishwa nchini kuwa jambo la Muungano na kutungiwa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, sura ya 147 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo kutokana na mageuzi mbali mbali wigo wa utozaji wa ushuru huu umetanuka na kuhusisha pia bidhaa zinazoingizwa kutoka nje ya nchi na kwa miaka ya karibuni kwenye huduma kwa maana *excise duty on services.*

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa taasisi na kwa kuzingatia jadweli la kwanza la Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya usimamizi wa mambo ya Muungano, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa imetoa uwezo kwa Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (*TRA*) ya kusimamia ushuru huo.

Kwa upande wa Zanzibar *ZRB* imekuwa ikisimamia ushuru huo kwa huduma zinazotolewa hapa Zanzibar ikiwemo kwa sekta ya benki. Hata hivyo, kumejitokeza utata juu ya uhalali wa *TRA* kusimamia ushuru huo kwa bidhaa zinazoingizwa nchini na kwenye huduma, na pia utata huo upo kwa *ZRB* kusimamia kwa bidhaa zenye ushuru huo zinazotengenezwa hapa nchini.

Madhumuni na Muundo wa Mswada

Mhe. Mwenyekiti, Mswada wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa una madhumuni yafuatayo.

1. Kulinda na kuongeza mapato ya serikali yanayotokana na vianzio husika
2. Kuwa na msingi thabiti wa kisheria wa kusimamia ushuru huo
3. Kuimarisha mazingira ya uwekezaji nchini kwa kuondoa utata juu ya mamlaka ya usimamizi, utozaji na ukusanyaji wa ushuru huo katika maeneo tofauti na hivyo kuimarisha zaidi misingi ya utawala bora
4. Kuwepo fursa ya utozaji wa ushuru kulingana na hali ya kijamii na mazingira ya uchumi wa Zanzibar na sera zake
5. Kuipa mamlaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuweka viwango vitakavyopunguza matumizi na uingizaji wa bidhaa zenye athari kwa mtumiaji.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada wa Sheria inayopendekezwa umegawika katika sehemu kuu tano zifuatazo.

Sehemu ya kwanza ya mapendekezo ya sheria hii inaelezea utangulizi na inahusisha vifungu vitatu vinavyohusiana na jina fupi la sheria na kuanza kutumika, utangulizi na tafsiri ya maneno yaliyotumika katika sheria hiyo.

Sehemu ya pili ya sheria inaelezea wajibu na utozaji wa ushuru wa bidhaa na huduma na ina vifungu 12 vinavyohusiana na utozaji wa ushuru wa bidhaa na huduma, muda na wajibu wa

kutoza ushuru wa bidhaa, sehemu za utoaji wa huduma zinazopaswa kutozwa ushuru, ukabidhishaji wa madaraka na uwezo, thamani ya utozaji wa ushuru, upimaji wa thamani ya kodi, vipimo vya kutathmini bidhaa na huduma, muda wa utoaji wa huduma na bidhaa zinazoingizwa nchini, muda wa kulipa ushuru, wajibu wa kulipa ushuru, bidhaa na huduma ambazo hazistahiki kutozwa ushuru na udhibiti wa utozaji wa ushuru wa bidhaa.

Sehemu ya tatu ya sheria inaelezea ulipaji wa ushuru na ina vifungu vinane vinavyohusiana na malipo ya ushuru, kiwango cha ushuru, thamani ya utozaji wa ushuru wa bidhaa kwa huduma zinazotozwa ushuru, mabadiliko kwa kushuka kwa kiwango cha tozo, mtu anayehusika kulipa ushuru wa bidhaa, ugomboaji, misamaha kwa ushuru wa bidhaa zinazoingizwa kwa kusafirishwa nje ya nchi na misamaha kwa bidhaa zilizobakia njiani wakati wa usafirishaji.

Sehemu ya nne ya sheria inaelezea hesabu na kumbukumbu na ina kifungu kimoja kinachohusiana na hesabu.

Na sehemu ya tano ya sheria kinaelezea mambo mengine ya jumla na ina vifungu 18 vinavyohusiana na kuingizwa tena kwa bidhaa kutoka nje ya nchi, udhibiti wa forodha kwa bidhaa zinazoanishwa, uingizwaji wa bidhaa zilizoanishwa kutoka nje ya nchi, uteuzi wa maeneo ya uingizwaji wa bidhaa, uingizwaji wa bidhaa zilizoanishwa kwenye ghala na uteuzi wa wakala.

Mhe. Mwenyekiti, mambo mengine yaliyomo katika sehemu hii ni pamoja na muda ambao bidhaa zitajuulikana kuwa zimeingizwa nchini, bidhaa zilizoingizwa nchini kupitia vifurushi vya posta, wajibu wa mtu anayestahiki kulipa ushuru wa bidhaa wakati ambapo hayupo Zanzibar, uhaulishaji wa umiliki kwa dhamana, mkopo au pendekezo la kuweka bidhaa ghalani, utaratibu wa ukiukwaji ulipaji kodi, maombi ya sheria ya forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, adhabu na makosa, kanuni, indhari na wajibu wa muingizaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru.

Mhe. Mwenyekiti, ili kurekebisha utata uliojitokeza hivi sasa juu ya taasisi ya kusimamia ushuru huo, mswada unaopendekezwa wa sheria ya ushuru wa bidhaa utaweka bayana mamlaka ya *ZRB* na *TRA* juu ya kusimamia na kukusanya ushuru huo. Hatua hii inatarajiwa kusaidia kuongeza au kuongezeka kwa zaidi mapato ya ndani na kuondoa kasoro ya baadhi ya walipa kodi kukaidi kulipa ushuru huo *ZRB* na wengine kukaidi kulipa ushuru huo *TRA*.

Mhe. Mwenyekiti, mswada unaopendeka kwa *ZRB* ikusanye ushuru wa bidhaa kwenye huduma zinazotozwa ushuru huo wakati kwa sababu ya kuhakikisha ufanisi kwa walipa kodi na wakusanyaji wa ushuru huo jukumu la kukusanya kwa bidhaa zinazotoka nje zitakasimiwa kwa Idara ya Forodha ya *TRA* ambapo kisheria ndio mdhibiti wa bidhaa zote zinazoingia nchini. Utaratibu kama huo unatumika pia kwa ada ya biashara *Trade Levy*, kodi ya ongezeko la thamani *VAT* na umefanya kazi vizuri bila ya matatizo tokea miaka ya 1990.

Hitimisho

Mhe. Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe, waupokee na kuujadili mswada huu na hatimae kukubaliana na mapendekezo ya mswada huu na kufanya tuwe na sheria mpya ya ushuru wa bidhaa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar (Kny. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kusoma hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuweka Vifungu vya Uanzishaji wa Kodi itakayojuulikana kama Ushuru wa Bidhaa na Huduma zinazoingizwa na Mambo Mengine yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kama ilivyo ada naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu ambaye hadi leo anaendelea kutujaalia neema zake ikiwemo neema ya uhai na afya mpaka tukaweza kutekeleza majukumu yetu, namuomba azidi kutujaalia neema hizo ambazo kwa hakika sote ni wahitaji kwake.

Mhe. Mwenyekiti, napenda pia kukushukuru na kukupongeza wewe pamoja na wasaidizi wako Mhe. Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza kwa namna mnavyoendesha Baraza kwa umahiri mkubwa, namuomba Mwenyezi Mungu awazidishie hekma na busara katika jukumu lenu la kutuongoza, ili tuweze kutekeleza vyema wajibu wa chombo hichi.

Mhe. Mwenyekiti, siwezi kuwasahau Wajumbe wa Kamati yangu ya Bajeti katika kuwashukuru kwa namna wanavyonipa mashirikiano makubwa, katika kutekeleza majukumu ya Kamati yetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu niwatambue Wajumbe hao kama ifuatavyo.

1.	Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa)	Mwenyekiti
2.	Mhe. Bahati Khamis Kombo	M/Mwenyekiti
3.	Mhe. Shehe Hamad Mattar	Mjumbe
4.	Mhe. Abdalla Ali Kombo	Mjumbe
5.	Mhe. Zulfa Mmaka Omar	Mjumbe
6.	Mhe. Simai Mohammed Said	Mjumbe
7.	Mhe. Asha Abdalla Mussa	Mjumbe
8.	Ndg. Abdalla Ali Shauri	Katibu
9.	Ndg. Kassim Tafana Kassim	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila iwapo sitotambua mchango wa wadau mbali mbali waliofika mbele ya kamati yangu, kwa dhamira ya kutoa maoni yao kuhusu Mswada huu ambao upo mbele yetu. Hivyo, kwa dhati kabisa, kamati yangu inawashukuru wadau hao kwa michango yao mizuri ambayo naamini itasaidia sana katika kuufanya Mswada huu kuwa bora zaidi. Aidha, napenda kuwahakikishia kwamba maoni na ushauri wao umezingatiwa na kamati yangu wakati ilipokaa na serikali, ili kupatiwa ufafanuzi kuhusu Mswada huu.

Uchambuzi wa Mswada

Mhe. Mwenyekiti, lengo la Mswada huu ni kuweka mfumo wa kisheria wa utozaji na ukusanyaji wa ushuru kwa huduma na bidhaa zinazoingizwa ndani ya Zanzibar, ambapo kwa sasa ushuru

wa bidhaa na huduma zinazoingizwa Zanzibar unakusanywa kwa mujibu wa Sheria ya Ushuru iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, tunaelewa kwamba kulipa kodi ni wajibu wa kila mwananchi. Hata hivyo, ni vyema kwa Serikali wakati wa kuanzisha kodi, ikazingatia upande wa pili wa shilingi yaani walipa kodi, badala ya kuaangalia upande mmoja tu wa kuongeza mapato, kwa kuwawekea mazingira mazuri yatakayomuwezesha mlipa kodi asione sifa kukwepa kulipa kodi. Hili sio tu kujenga mahusiano mazuri baina ya pande hizi mbili, lakini pia litahamasisha kulipa kodi kwa hiari. Aidha, ili kulinda wajasiriamali wa ndani, kamati yangu inaishauri serikali iangalie uwezekano kwa bidhaa zinazozalishwa kwa malighafi za ndani, kodi zake zitozwe kwenye uuzaji badala ya kutoza kwenye uzalishaji.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu imefarijika sana na uamuzi wa serikali kuja na mswada huu, ambao utaipatia serikali nguvu za kisheria pamoja na fursa ya kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato. Kwa kuwa Kamati yangu ya Bajeti ina jukumu la moja kwa moja la kuishauri serikali katika kuibua vianzio vya mapato, tunatarajia kuwa kupitia sheria hii, itakuwa ni chachu ya kuongezeka kwa mapato ya serikali ambapo kabla ya sheria hii, serikali ilikuwa inakosa baadhi ya mapato yake kutokana na kutokuwa na nguvu za kisheria za kukusanya mapato hayo, ikiwemo eneo muhimu la huduma za mitandao ya simu ambalo kimsingi kwa sasa limeimarika sana.

Mhe. Mwenyekiti, kama ambavyo Kanuni zetu za Baraza zinatuelekeza napenda kukiri kuwa, kamati yangu ilipata fursa ya kuupitia mswada huu kwa kina na kutoa maoni yake kwa serikali, kwa dhamira ya kuifanya sheria itakayotungwa iwe bora zaidi na iweze kutekelezeka. Hivyo, kutokana na mapitio hayo, kamati yangu imependekeza baadhi ya marekebisho kadhaa katika vifungu mbali mbali. Baadhi ya marekebisho hayo ni pamoja na marekebisho ya kisarufi, ambapo vifungu mbali mbali vilirekebishwa kwa lengo la kuviwezesha kusomeka vyema na kuleta maana halisi iliyokusudiwa. Baadhi ya vifungu hivyo ni kifungu cha 3 cha Mswada, tafsiri ya neno “ungizaji” liliopo ukurasa wa 29 limerekebishwa na kusomeka “uingizaji”. Aidha, neno “kuingizwa” liliopo baina ya neno “kusababisha” na neno “kwa” limerekebishwa na kusomeka “kuingiza”, sambamba na kuongeza neno “ya” baina ya neno “ndani” na “Zanzibar”.

Mhe. Mwenyekiti, marekebisho mengine yaliyopendekezwa na kamati yangu yanatokana na makosa ya kiuchapaji, baadhi ya marekebisho hayo ni katika kifungu cha 23 cha Mswada, kwenye maneno ya pembeni ya kifungu hiki neno “nchi” limependekezwa lisomeke “nchini”. Aidha, neno “kuzisafirishwa” lililopo baina ya maneno “baada ya” na maneno “nje ya nchi” limependekezwa lisomeke “kusafirishwa”. Vile vile, neno “ikawa” liliopo mstari wa pili, baina ya neno “na” na “hakuna” limependekezwa lisomeke “ikiwa”. Katika mstari wa tano maneno “ikawa imeengezeka” yaliyopo baina ya neno “yake” na neno “kiwango” yamependekezwa yasomeka “kuongezeka”.

Mhe. Mwenyekiti, marekebisho mengine yaliyopendekezwa na kamati yangu ni kuweka usawa wa maneno baina ya Mswada wa Kiswahili na Mswada wa Kiingereza ili Miswada hii iendane. Mfano wa vifungu vilivyorekebishwa ni kifungu cha 5 na 6 cha Mswada, ambapo katika vifungu hivyo, maneno “kiwango cha” yanafutwa na kusomeka “thamani ya”. Aidha, katika

kifungu cha 28 maneno ya pembeni yanarekebishwa na kusomeka kama ifuatavyo: “Mfumo wa kuepuka kulipa kodi”.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kamati yangu ilipependekeza marekebisho ya kufuta na kuandika upya baadhi ya vifungu ambavyo vilikuwa na utata. Mfano wa vifungu hivyo ni kifungu cha 9(2) cha Mswada ambacho kimependekezwa kuandikwa tena ili kisomeke kama ifutavyo:-

“Mtu ambaye atachukua au atajaribu kuchukua bidhaa zinazotozwa ushuru zikiwa chini ya udhibiti wa forodha ataadhibiwa kwa kulipa mara mbili ya ushuru unaopaswa kulipwa kwa bidhaa hizo”.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu pia ilipendekeza kufutwa kwa baadhi ya vifungu vya Mswada huo ambavyo vilionekana havina msingi wowote. Baadhi ya vifungu hivyo ni pamoja na kifungu cha 26 cha Mswada. Mhe. Mwenyekiti, marekebisho ya ziada yapo kwenye Waraka wa Kamati wa Mapendekezo ya Marekebisho ya Mswada huu, ambao naamini Wajumbe wamepatiwa.

Hitimisho:

Mhe. Mwenyekiti, naamini Wajumbe wa Baraza lako wamepata fursa ya kuupitia kwa kina Mswada huu na kubaini maeneo kadhaa ya kuishauri serikali kuhusu utekelezaji bora wa Sheria inayotarajiwa kutungwa. Hivyo, ni matumaini ya kamati yangu kuwa Wajumbe wa Baraza hili watauchangia, wataujadili, na hatimae kuupitisha Mswada huu ikiwa ni sehemu ya jukumu la Baraza, na hatimae kuipa fursa serikali kutekeleza sehemu ya jukumu lake la utekelezaji wa Sheria itakayotungwa**.**

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Zulfa Mmaka Omar kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea na nina mchangiaji mmoja mpaka hivi sasa naye nimuite Mhe. Rashid Makame Shamsi. Waheshimiwa Wajumbe nafasi ipo majadiliano yanaendelea kama kuna mwengine alete. Kwa hiyo, Mhe. Rashid Makame Shamsi naomba uendelee.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana. Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya mwanzo sasa kuweza kuchangia mswada huu uliopo mbele yetu unaohusiana na Sheria ya Ushuru wa Bidhaa na Huduma ya Mwaka 2017.

Mhe. Mwenyekiti, nianze vile vile kwa mara nyengine kuweza kumshukuru na kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kufikiria, kuweza kuleta mswada huu wa dharura kwa lengo lile lile la kuweza kuhakikisha kwamba tunadhibiti mapato na uchumi wa visiwa hivi unakua siku hadi siku. Lakini vile vile nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa kazi nzito anayoendelea kuwa nayo katika Baraza hili na miswada mingi sana ambayo inamuhusu na nampa moyo kwamba aendelee kuisimamia vyema.

Vile vile niwapongeze kamati inayohusiana na bajeti kwa kazi kubwa ambayo wameifanya ya kuweza kuipitia miswada hii ukiwemo huu na hatimaye kupendekeza marekebisho kwa lengo la kuweza kuufanya mswada huu uwe bora zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze sana serikali kwa kuweza kuona kuna kasoro za ulipaji wa kodi hii ya bidhaa zinazoingia Zanzibar, niseme kwamba tumechelewa sana kwa sababu tulikuwa na vilio vya muda mrefu juu ya suala hili. Tumechelewa kwa sababu malipo haya yalikuwa yanalipwa katika ile Sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hivyo inawezekana kwamba Zanzibar tulikuwa tunakosa mapato, lakini kuliona hili kwamba sasa umefika wakati kuweza kuunda sheria, nafikiri ni wazo zuri na litafanya sasa zile bidhaa zinazoingia Zanzibar basi mapato yake yaingie katika Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar. Napongeza sana katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, sheria hii kama tulivyosema ilikuwa haipo na tulikuwa na sheria moja ya Muungano, sasa wasiwasi wangu kidogo tu kwamba wafanyabiashara wetu walikuwa wameshazowea kwamba wanalipa kwa mujibu wa sheria ile ya Muungano sasa kuna sheria hii ya Zanzibar. Sasa waziri atakapokuja labda aweze kutoa wasiwasi kwa wafanyabiashara na wananchi juu ya hili, ili isije ikatokea sasa misongomano kutoka yale mazowea ya mwanzo na sasa kuingia katika sheria hii mpya ya Zanzibar, lakini waelewe tu wenzetu kwamba lengo ni kuona mapato yale ya bidhaa zinazoingia Zanzibar basi yanaingia katika Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hilo ningependa Mhe. Waziri aje aliweke sawa ili wananchi wasiwe na wasi wasi na hilo, lakini vile vile taaluma inahitajika kwa sababu ya mazowea ambayo yalikuwepo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiingia katika Mswada wenyewe ukurasa wa 26 nasisitiza suala lile lile la kuyaweka maneno yaliyofafanuliwa katika utaratibu mzuri, lakini nikija katika ukurasa wa 28 katika neno la chini kabisa linalosomeka 'kusafirisha nje ya nchi' na maana yake, basi ningependa tu na mimi kuweza kutoa mapendekezo hapo kwamba isomeke, 'maana yake kunahusiana na', hiyo 'katika kuhusiana', mimi nataka ikae kama 'kuhusiana na'.

Vile vile kipengele cha (a) pana maneno 'bidhaa ni uchukuaji'. Hilo neno ningependa libadilike na liwe 'uchukuaji wa bidhaa', yaani *goods to take*. Lakini (b) maneno yaliyoanza na mstari huo ni usambazaji, kwa tafsiri au muktadha wa *service to supply service*. Ningependa tufanye marekebisho isomeke, 'huduma katika usambazaji huduma', kwa muktadha wa "*service to supply service"*.

Mhe. Mwenyekiti, nije ukurasa wa 29 katika neno lililotafsiriwa 'nchi washirika', ni neno la tatu kutoka chini. Maana yake imeelezwa hapa kwamba, "ni nchi yoyote iliyopewa uanachama chini ya ibara ya 3 ya mkataba wa uanzishaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki". Ningependekeza hii ibara ya 3 ya mkataba huu, huu mkataba uainishwe ulikuwa ni mkataba wa mwaka gani, kama ni mkataba wa mwaka 2004 basi uwekwe wazi, kwa sababu inawezekana kulikuwa na Jumuiya ya nyuma huko. Sasa tuweke uwazi kabisa kwamba huu ni mkataba wa mwaka kama ni 2004 au vyenginevyo, lakini ni vyema uwepo wazi.

Halafu kwenye neno 'spirit' sidhani kama wenzetu wamerekebisha, lakini kuna maneno hapo 'yeyote na inajumuisha'. Nataka nifanye marekebisho isomeke 'yoyote' na sio yeyote na inajumuisha.

Mhe. Mwenyekiti, tukija katika ukurasa wa 30 katika tafsiri ya neno 'chombo' nilikuwa ninapendekeza tafsiri hiyo ibadilike kidogo na isomeke 'chombo kinajumuisha kila aina ya chombo cha usafiri kinachotumika na mtu yeyote'. Nilikuwa napendekeza hivyo kwa sababu hili neno 'aina ya usafiri' aina za usafiri ziko nyingi na wakati mwengine tuna usafiri mpaka wa punda. Sasa nafikiri tungeweka vizuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 31 katika kifungu cha 8(2)(c), pana maneno yanayosema 'imeondolewa maeneo huru'. Katika muhtadha wa Kiingereza inasema *"removed from an export processing zone"*, sidhani kama hilo neno lililowekwa litakuwa na muhtadha huo, ningependa litazamwe vyema ikiwezekana kuweza kuweka sawa.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nije katika ukurasa wa 34 katika kifungu (d) ambacho kinasomeka 'tozo au ada zilizokusanywa na taasisi za fedha au watoa wa huduma'. Ningependa hilo neno 'watoa' liondoke lisomeke 'mtoa huduma, taasisi za fedha au mtoa huduma', kwa maana ya *service provider* ambayo inasomeka katika *version* ya Kingereza. *Service provider* isomeke hivyo. Lakini vile vile tukiangalia katika kifungu hicho hicho cha (d) katika mstari wa tatu limeandikwa neno 'utoaji wa huduma'. Hapa ningependa hilo neno liondoke na baadae liwe 'uhaulishaji wa huduma' kwa muhtadha ule wa *transfer service* ambayo iko katika *version* ya Kiingereza, *is not produce service* lakini iko katika *transfer service*, yaani uhaulishaji wa huduma.

Tukija katika kifungu cha 14 ukurasa huo huo ambapo kama nilivyosema pale nyuma pana kifungu (a) kinachosema kwamba, 'uingizaji wa bidhaa nchini zinazotozwa ushuru kwa mujibu wa masharti ya sheria ya usimamizi wa forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki'. Hii sheria ni vyema iainishwe mwaka gani, hiyo sheria inayohusiana na usimamizi wa forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili iwe wazi, yaani mtu akitaka kuipitia basi asipate tabu kuliko hivyo ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika ukurasa wa 37 kuna kifungu cha 4(a) imetajwa hapo 'kuvunja au kufungua mlango au dirisha au kuvunja ukuta'. Tukirudi katika *version* ya Kingereza basi ni vyema isomeke, 'kufungua mlango wowote, *any door*; lakini vile vile kuvunja ukuta wowote, *any wall*.

Nikija katika kifungu (b) ambacho kinasomeka 'kuvunja eneo la chini au sakafu ya eneo lolote kwa madhumuni ya kufanya ukaguzi...', hilo neno 'ukaguzi' ningependa ligeuke kidogo hilo liwe neno 'upekuzi' kutokana na muhtadha wa neno *search* kama tulivyozowea na kwa sababu hapo kitendo kinachofanywa sio ku-*inspect* lakini ku-*search*. Hapo kwa Kiswahili chetu kizuri ingekuwa ni upekuzi.

Mhe. Mwenyekiti, neno hilo hilo la upekuzi nataka litumike katika kifungu cha 6(a) ukurasa wa 38 mstari wa tatu neno la sita ambalo limetumika ukaguzi wa chombo.

Mhe. Mwenyekiti, tukiondoka hapo nije sasa katika ukurasa wa 40 katika kifungu cha 27(d) mstari wa pili kutoka chini ambapo inasomeka 'kulipa ushuru kwa niaba yake kana kwamba', imesema neno 'kana kwamba', hakuna neno kana kwamba isomeke 'kama kwamba'. Lakini neno hilo hilo 'kana kwamba' limetumika katika kifungu cha 28 mstari wa pili kutoka chini neno la pili kutoka mwisho imetumika tena "kana kwamba" lisomeke "kama kwamba".

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 41 katika kifungu cha 31. Hapa Mhe. Mwenyekiti, imeeleza zile adhabu ambazo anaweza kuzipata huyu mtu ambaye amefanya makosa haya ma ushuru. Katika kifungu cha (a) mpaka kifungu (g) halafu ikasema kwamba atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini mara mbili ya ushuru unaopaswa kulipwa au kifungo cha kipindi kisichopungua miezi mitatu au kisichozidi miezi sita au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Lakini kifungu cha pili napo vile vile pana adhabu sasa hichi kifungu cha pili adhabu yake mimi naiona kubwa kuliko hii adhabu ya vifungu hivi kuanzia (a) mpaka (g). Sasa nafikiri tuitizame vizuri Mwanasheria kwa sababu inawezekana huyu wa vifungu hivi vilivyotangulia juu akaja akalipa faini ndogo sana kuliko huyu ambaye yuko katika kifungu cha pili. Tungeitizama vizuri hayo makosa yaliyotajwa hapo na tuweze kuona kwamba tunatenda haki na hizo adhabu ziwe zina uwiano.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika ukurasa wa 42 vile vile kulikuwa na *concern* ambayo nilisema nyuma masharti ya sheria ya usimamizi wa fedha ya jumuiya ningependa iwekwe hiyo sheria ni ya mwaka gani, ili iwe wazi zaidi. Lakini nikija katika kifungu cha 34(2)(e) ambacho kimeanza na maneno kuwainisha kuna neno hapo "linalotakiwa" neno la kwanza mstari wa pili lingesomeka "linatakiwa" ambalo linatakiwa kuelezwa sio linalotakiwa. Halafu kifungu cha 35 neno la tatu jambo lolote "lilofanywa" ningependa lisomeke "lililofanywa" nafikiri linaweza likaa vizuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mswada huu mimi mchango wangu zaidi ni huu ambao nafikiri unaweza ukasaidia katika kuufanya uwe bora zaidi na niwaombe tu wenzangu nao waweze kutoa michango yao ili kuufanya mswada huu uweze kupitishwa vizuri. Mimi niseme tu naunga mkono asilimia kwa mia mswada huu tuupitishe ili sheria hii ianze kutumika. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii tena mara ya pili kuchangia mswada ulio mbele yetu.

Mimi mchango wangu kwa hapa moja kwa moja utakuwa ni mchache lakini ni yale yale namsihi sana waziri wetu.

Niendelee kupongeza Mhe. Rais wetu mpendwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kutuletea chombo kama hichi tuweze kupitisha kwa haraka kwa vile ni mswada wa dharura ili uweze kufanyakazi na uweze kuleta tija iliyokusudiwa. Lakini pia vile vile nimuombe Mhe. Rais nae pamoja na majuku aliyonayo mengi kama vile ilivyoletwa kwa dharura miswada hii basi na yeye afanye kwa dharura kuisaini haraka ili ifikapo Julai nayo iweze kufanyaka kazi tuweze kukusanya

mapato kama inavyokusudiwa tuweze kutekeleza majukumu yetu katika mwaka 2017/18 na kuendelea.

Mimi katika mchango wangu nitachangia katika hotuba ya Mhe. Waziri sehemu ya 5 ya sheria hii inapoeleza kwamba mambo mengine ya jumla na ina vifungu 18 vinavyohusiana na kuingizwa tena kwa bidhaa kutoka nje ya nchi, udhibiti ya forodha kwa bidhaa zinazoainishwa. Uingizwaji wa bidhaa zinazoainishwa kutoka nje ya nchi na uteuzi wa maeneo ya uingizwaji wa bidhaa.

Mhe. Mwenyekiti, hapa Mhe. Waziri aelewe kwamba ndipo sehemu ambapo kuwa tunatiwa changa la macho tena kwamba bidhaa zinaingia kutoka nje ya nchi. Lakini ukifika wakati wa kukagua makontena pale bandarini hapa ndio pale pale kuna watu hawawezi kuishi bila ya kujaza mifuko yao kinyume cha uhalali.

Namueleza tena Mhe. Waziri kwamba sehemu za bandarini ndio sehemu ambazo tunategemea uchumi wetu kunyanyuka kwa hali ya juu sana mapato mengi nchini. Lakini ndio pia pahali ambapo kuwa watu wanajinufaisha kwa maslahi yao binafsi baada ya maslahi ya umma. Leo linaweza kuja kontena pale kutoka nje karani anaambiwa nenda kakague kontena utakuta *document* ina vitu vyengine na kwenye kontena kuna vitu vyengine, ili akiona kwamba vitu vilivyokuwemo kwenda kontena ni vitu ambavyo kuwa vina bei hafifu.

Lakini kumbe vitu vilivyokuwemo ndani ya kontena ni vitu vya thamani kubwa ambavyo vinapaswa kutozwa ushuru kama inavyostahili. Ujanja unaopatikana hapa ni kwamba anaekwenda kufungua kontena akifika anaona hati ilivyo na kilicho humo ndani ya kontena ni tafauti hata akirudi kwa bosi wake kumuuliza hebu mbona umenambia nikakugue nikaangalie biskuti mbona kuna vitu vyengine haambiwa wewe hutaki kazi au hutaki kula wewe hichi kinafanyika Mhe. Waziri hilo ukielewe.

Kwa hivyo, watu kama hawa wamo katika sehemu zetu za forodha na ndio wanaikosesha mapato nchi yetu matokeo yake wao wanajilimbikizia mali kinyume na taratibu. Tuwaone sana bado kuna watu hawawezi kuishi bila ya kudokoa au bila ya kula na wengine wanakula bila ya kunawa.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika mchango wangu mimi mwengine alipozungumzia suala la bidhaa zinazongizwa nchini kupitia vifurushi vya Posta. Hapa Mhe. Waziri tusiangalie kwa njia ya Posta tu, kuna vifurushi na sehemu mbali mbali ambazo kwa taasisi mbali mbali zimejitokeza kwa hivyo tuziangalie sana sehemu kama hizi ambazo zinaweza kupata mapato katika kusaidia pato la nchi yetu.

Kwa hivyo, ni jambo muhimu sana kufumbua macho yetu tukaangalia ni taasisi gani nyengine zinazotumia kuingiza mambo yao kusafirisha, ukiachia Posta. Sasa hivi Posta ni sehemu ndogo sana ambayo inatumika kwa kupitisha bidhaa, taasisi nyingi sasa hivi zimeanzisha kwa mfano utaona sasa watu wanasafirisha pesa kwa njia namna mbali mbali na baadhi ya vitu vyengine. Kwa hivyo, tuwe wagunduzi sana wa kuzitafuta ni zipi na zipi tumeona kwamba zitaweza kutusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja hii nilikuwa nipate nafasi tu nimtanabahishe Mhe. Waziri na kuwaomba sana watendaji bado waliokuwa hasa bandarini na sehemu za viwanja vya ndenge wawe waaminifu. Kwani kila mwenye kutaka utajiri Mjumbe au Mtume wetu Muhammad (*SAW*) amesema "kukinai kunamtosha".

Kwa hivyo, tuwe na kinaa wanaowekwa sehemu ambazo kuwa kuna mapato ya nchi yetu tusiweze kujilimbikia sisi wenyewe tujali maslahi ya umma baada ya yetu binafsi. Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii mia juu ya mia. Ahsante sana.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kidogo maneno mawili mswada huu. Mswada ambao unajitosheleza lakini kidogo na sisi tunataka tutie tie nyama kwa baadhi ya mambo ili yaende vizuri.

Kwanza, mimi sina budi kumpongeza sana Waziri na timu yake kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuupitia mswada huu kwa sababu ni kilio chetu sisi Wawakilishi siku nyingi juu ya kufanyiwa marekebisho haya ya kodi. Wenzangu waliotangulia walisema kwamba na yeye mwenyewe waziri kaeleza vizuri kwamba kodi tulizonazo katika Mswada huu wa Sheria ni bora kuliko zile zilizotangulia kutona na viwango vyake na mimi nakubaliana nae. Kabla ya yote nasema naukubali mswada huu kwa asilimia mia na naunga mkono kwa asilimia mia. Lakini nilikuwa naomba kidogo tuongeze nyama ili kuuweka sawa baadhi ya mambo.

Mheshimiwa mimi kidogo Mwenyekiti naomba niingie katika ukurasa wa 37 kifungu cha 4 naomba nikisome kidogo hicho kifungu kinasema:

"Endapo afisa aliyekasimiwa au afisa aliyeidhinishwa, na baada ya kubainisha uwezo wake na madhumuni yake kwamba anahitaji kuingia ndani ya eneo lolote na endapo muda ule hakuruhusiwa kuingia yeye na msaidizi wake, anaweza muda wowote isipokuwa wakati wa usiku awepo Afisa wa Polisi".

Hapa nataka nichangie kidogo kwanza lile neno "uwezo" lililopo baina ya kubainisha na yale madhumuni lile neno "uwezo". Mimi nilitaka lisomeke neno "cheo" liwe ni "cheo". Kwa sababu ukisema uwezo hata mimi nina uwezo wa kwenda lakini "cheo" changu ni kipi. Kwa hivyo, pale kisemwe kwamba baada ya kubainisha cheo chake mfano aah! mimi nielikuja hapa ni Afisa wa *ZRB* au ni Afisa wa *TRA* kitu kama hicho unaona akathibitika kama yeye ndie. Sasa ndio aendelee na hiyo kazi yake isiwe uwezo, uwezo anao mtu yoyote hata majambazi wanao uwezo kwa kwenda mle wakavunja. Kwa hivyo, abainishe hili neno uwezo liandikwe cheo au nafasi yake ya kazi aliyonayo litafutwe neno zuri baada ya hili neno "uwezo", hilo la kwanza.

Lakini la pili mwisho wa hiyo sentensi nilikuwa napenda liongezwe neno tungetajwa hicho cheo cha huyo Afisa ya Polisi, ikisha kama ni wakati wa usiku kama alivyosema angekuweko na Sheha kwa ajili ya kuweka tukamtaja kwenye sheria kwa sababu ya kuweka usalama zaidi wa yale mambo yanatakayokwenda kufanyika pale. Kwa sababu ukenda kwenye hiyo ibara ya 30 imetajwa mpaka uwezo wa kuvunja ukuta, tukienda katika ibara ya 30 Mheshimiwa tutaikuta hiyo kwamba tunataka tuwape uwezo mpaka wa kuvunja ukuta.

Sasa kuifananisha kwa sababu hiyo mimi ningekuwa napendekeza kwamba suala hili la kuvunja tungeliangalia vizuri na tusingeliwekea kama ni askari tu yoyote kama mwenye uwezo wakati wa usiku wa kwenda na kutaka kuvunja. Kwa sababu tukivunja kama ukuta itakuwa ile sehemu iko wazi, sehemu ikiwa wazi mwizi anaweza kupita pale akishapita mwizi itakuwa sasa hatujafanya chochote bado tunaongeza matatizo baada ya kupunguza matatizo sasa tunaongeza.

Sasa ili tuepuke yale matatizo kwanza mimi nilikuwa sipendekezi kwamba kuvunjwe ukuta hili neno ukuta lisitajwe iwe ni kuvunja mlango au dirisha jambo ambalo tunaweza kulimiki na ikawa mtu mwengine hapati kupita. Au kama ni ukuta uandikwe uainishwe ni ukuta upi tuseme mfano wa wa ghala au kama ni wa *fence* sawa. Lakini si ukuta wa kuingia ndani ya ile ghala ambayo ina mali baada yake tukenda kujitafutia matatizo yaliokuwa tunaweza kuyaepuka. Kwa sababu mtu tukimvunjia ukuta wa duka pale inaweza ikatokea rapsha watu wakenda wakaiba wakaenda mahakamani na wakishafika mahakamani sasa ikawa kesi nyengine sasa itayotukabili. Sasa pale mimi napendekeza kwamba lile neno la "ukuta" pale tuliondoe.

Tukija katika kifungu cha 28 kwenye ukwepaji wa kodi. Mimi nilikuwa nikipenda iwekwe wazi kwamba mtu alieshindwa kulipa kodi ikibainika kama ilivyoelezwa aweze sheria itaje kwamba ailipe kodi ile ndani ya miaka yote mitano au kwa muda wote wa ile biashara iliyobainika kwamba yeye amekataa kulipa ile kodi ya serikali. Asikadiriwe ikiwa kodi yake ilikuwa ni shilingi milioni moja ndani ya mwezi alipe kwa muda wote ambao yeye kakwepa maana yake kaiba yule kodi ile ni mali ya serikali ni mali ya wananchi wa Zanzibar. Kwa hiyo, yeye kaichukuwa peke yake airejeshe kwa wenyewe, hili mimi nilikuwa napendekeza liwekwe wazi.

Ikisha katika hiyo 30 ndiyo imejirudia kwa kuhofia lile ambalo nimezungumza kule nyuma. Kwamba mtu ambaye atajifananisha na afisa aliidhinishwa au aliekasimiwa madaraka kifungu hiki ndio nilikuwa nakitilia mkazo kwa yale maelezo yangu ya nyuma kwamba tusije tukatoa *room* kwa mtu mwengine akajifananisha yeye kama ni Afisa wa Kodi akenda akaweza kufanya ubadhirifu kama huyo.

Lakini pia katika kifungu cha 31(e) na (f) makosa na adhabu, anasema mtu ambaye katika kifungu (e) atashindwa au atakataa kutoa nyaraka au maelezo yanayotakiwa kuhusiana na bidhaa au huduma na biashara zinazopaswa kulipiwa ushuru na (f) atashindwa kujibu maswali aliyoulizwa na afisa aliyekasimiwa au afisa aliyeidhinishwa. Hapa nilikuwa nina mapendekezo yangu naomba tuyaangalie sana. Sisi Zanzibar tuna tabia moja ambayo si kilema lakini ni tabia yetu ya kawaida mtu anaweza kuliacha duka lake au sehemu yake ya biashara akamuachia mwenzake akawambia nishikie niangalizie mimi biashara yangu hii naenda msikitini kusali, akaja kutokea Afisa wa Kodi akataka maelezo pale.

Sasa yule mtu maelezo ya pale hayajui na sheria tayari imeshamfunga tumeshamtia hatiani tutafanyaje? Kifungu hiki kwa maoni yangu mimi naona napendekeza kwamba iwapo atashindwa pale kupewa maelezo duka lile lifungwe mpaka atakapokuja muhusika mwenyewe au kama ni afisi vile vile zidhibitiwe tusibiri maelezo ya mwenyewe muhisika kwa muda maalum tumpe muda maalum kama ni siku tatu au nne kumtaka mwenyewe aje pale ajibu maswali atakayoulizwa na Afisa anaehuika. Kwa hili tukilisema tu moja kwa moja kwamba mtu

atakaekuwepo katika sehemu ile inayohitajika kulipa kodi akiulizwa maswali akishindwa kujibu kumtia hatiani tutakuwa hatujatenda haki.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi mswada nauunga mkono kwa asilimia mia na nawaomba wenzangu wote tuunge mkono kwa sababu ni mswada unaojitosheleza. Lakini nafikiria sana na naomba sana haya yazingatiwe hasa hivi vifungu vya mwisho vya (e) na (f) kutokana na mazingira yetu ili tuweke hali ya uwiano tusione wananchi wetu pamoja na kuwa wafanyabiashara ni wababishaji lakini kidogo kidogo tusije tukaingia katika mambo ambayo hayatakuwa wenye kupendeza sana.

Baada ya haya Mhe. Mwenyekiti, natamka kwamba naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Omar Seif Abeid kwa mchango wako Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuendelea na majadiliano kuna taarifa ya msiba ambayo Waheshimiwa sote tunapewa taarifa hiyo kwamba Mhe. Khatib Suleiman Bakar ambaye alikuwa Mwakilishi wa Jimbo la Bububu na Naibu Waziri wa Wizara ya Kilimo 2005/2010 amefariki dunia, maziko yatakuwa leo saa 7 mchana Mwanyanya. Ahsanteni.

Tunaendelea Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana na Wanawake na Watoto na Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, naomba niungane na wenzangu wote ambao waliotangulia kumpongeza Mhe. Waziri kwa ajili ya kuleta mswada huu mbele yetu.

Nipende pia kuwapongeza watendaji wote wanaokuwa wanaoandaa hizi taarifa kabla hazijafika hapa ikiwa pamoja na Dkt. Abdulhamid Mzee Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi kwa maandalizi ya taratibu wanazokuwa wanatuletea. Lakini pia na wachapaji wetu wa viwanda vya uchapaji ambavyo vinatuletea. Sasa hivi uchapaji wao umekuwa ni mzuri.

Pia niseme nawashukuru Katibu wa Baraza la Wawakilishi pamoja na ofisi yake yote, naamini wanafanyakazi usiku na mchana katika kipindi hiki, kwa hivyo na kazi wanazifanya kwa umakini.

Mhe. Mwenyekiti, nisingependa kuchangia mengi isipokuwa napenda pia kumpongeza Mhe. Waziri wa Fedha na MIpango kwa kazi zake, naona safari hii amekuwa yeye ndio mwenye kazi nyingi sana, kwa sababu ameanzisha mambo mengi mapya pamoja na msaada wa Wanasheria Wakuu na ofisi zao katika kazi za kuhakikisha kwamba miswada yote inayoletwa hapa ni ile ambayo imepitiwa kwa *interest* ya serikali na pia kwa *interest* ya wananchi, ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inakwenda katika mtakabala mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, ningependa kuchangia katika ukurasa wa 37 (a) na (b) kwa ajili ya ofisa kuingia mahali popote kwa ajili ya ukaguzi. Nilimsikia mwenzangu ameyazungumza hayo kusema kwamba labda katika suala la kuingia iwe na utaratibu ambao unaweza kuwa ni mzuri

zaidi, najua atafanya hivyo. Lakini mimi sikuendea huko, nilikuwa nataka kukuonesha tu kwa kusema kwamba kumekuwa na tabia ya wafanyabiashara wengi au watu wenye biashara kutotaka kukaguliwa mara kwa mara. Mara nyengine mtu anaficha au anafunga mlango, lakini ikiwa kutakuwa na utaratibu ambao utaonesha kabisa kwamba anapaswa akaguliwe na akatii hawezi kulazimishwa kufanya kitu hicho.

Mhe. Mwenyekiti, nasema kwamba sidhani kama kutakuwa na raia yeyote ambaye atataka kukaidi ili kulazimisha mpaka ifike wakati wa kuweza kuvunja ukuta wa nyumba yake, itakuwa ni akili ambayo haipendezi, ni vyema awe ni mtii na ukiitii serikali basi unakuwa huna shida katika maisha yako. Kwa hivyo, ni kitu kizuri kwamba kama kutakuwa na kulazimisha basi alazimishwe na mtu atakayekuwa analazimisha aweze kuwa ni mtii wa kuweza kushirikiana na serikali kuhakikisha kwamba wanafanya ukaguzi wa kutosha kwa ajili ya mapato.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 39 kifungu cha 24 kinasema udhibiti wa forodha kwa bidhaa zinazopaswa kutozwa ushuru. Mhe. Mwenyekiti, ikiwa wafanyabiashara watakuwa waaminifu basi serikali itafanyakazi yake kwa urahisi zaidi. Wasiwe wanaonesha risiti moja wakati wana mambo mengi ambayo yamewekwa kwenye biashara zao, hasa hii itatusaidia pia sisi kujenga tabia ya kutunza risiti, maana yake imekuwa mara nyingi unakuwa unatunza unajua aa! nitasema maneno tu ya kubabaisha udhibiti wa risiti sio muhimu kwa sababu najua fulani na fulani wananifahamu kwa hivyo naweza kufanya hivyo. Lakini kama itakuwa *seriousness* tabia ya kutunza risiti itasaidia.

Mhe. Mwenyekiti, nakumbuka wazee wetu wametunza risiti hata za kuanza kuingia kwenye harakati mbali mbali. Leo hii anakuonesha hii nimeikata mwaka 1964, kwa hivyo kukiwa na sababu ya kutaka kuitumia anatumia na inamsaidia kwenye masuala mengine ya kuendeleza kufanya shughuli zake.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 41 inayohusiana na adhabu. Mimi naunga mkono kabisa kuwa adhabu hizo zilizotolewa, hasa pale zinapotolewa na angalau zimeoneshwa kwamba ni kubwa kidogo hapa. Faini ya watu wenye uwezo kuona ndio njia ya kurahisisha. Maana yake inapofikia kuwa faini ni ndogo, basi mtu mwenye uwezo anaona kuwa ataendelea kufanya makosa na nitatoa faini na nitatoka. Lakini kama kwa mfano kwa kiwango hicho ambacho kimesema hapa kinaonesha kwamba kitasaidia. Mtu akikosa katika ukurasa huu inasema kwamba anapaswa alipe kwenye milioni mbili na isiyozidi milioni 10. Pia kifungu hicho kinasema kifungo chake ni mwaka mmoja mpaka miaka mitano.

Mhe. Mwenyekiti, mimi napenda kuwashauri wanasheria, wanapokuja kwenye masuala haya ya kutoa hukumu, basi wasianzie zile hukumu za mwanzo mwanzo, waende kule kwenye *margin* za mwisho, ili kuweza kuwadhibiti watu wanaoona kwamba si atafungwa mwaka mmoja tu mpaka miaka mitano, kwa hivyo anasema anataka nitowe muda mfupi. Ni vyema akaweka kwenye *margin* kubwa ili kuhakikisha kwamba na watu wengine wasiweze kuchukulia mambo yasiyofaa.

Mhe. Mwenyekiti, pia kutoa nyaraka za uongo hii itasaidia kupunguza *forgery*, watu waliokuwa na tabia ya kuchukuwa na kuweka nyaraka za uongo halafu anajua mambo yangu yatakwenda tu.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 42 waziri anaweza kutangaza katika gazeti rasmi la serikali kutunga kanuni kwa utekelezaji mzuri wa masharti ya sheria, bila kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha namba 1, na kifungu hiki waziri anaweza kufanya mambo yafuatayo ambayo yana (a) mpaka (e). Hii inasaidia kuona kwamba waziri na yeye anaweza kuwa na mambo ambayo na yeye ni binadamu, anaona mambo ambayo anaweza kufanya ni mazuri na ambayo yatakuwa ni faida kwa wananchi.

Lakini la mwisho nataka kusema kwamba kwa kuwa tuko katika kutekeleza masuala muhimu ya kitaifa. Nchi yoyote inapoendelea tunapona kwamba maendeleo yanakuwa mazuri ni pale tu watu wanapotii na kuweza kutoa kodi. Sisi wenyewe mara nyingi tumekuwa wavivu tunapokwenda mahala labda unanunua hutaki kudai risiti unaona kama unamfanyia muhali yule mwenye duka au unaona kama unamfanyia *favour* kitu ambacho sio sahihi.

Mimi nimefurahishwa sana na wenzetu upande wa pili wameanza kutaka kuhakikisha kwamba sasa hivi suala la kufuatilia kwamba nani amenunua bidhaa, kuna watu watakaa nje ya milango, watakuweko masokoni na watakuwepo kila mahala kuhakikisha kwamba mtu ambaye atakuwa hajalipa ataulizwa hebu tuoneshe bidhaa uliyonunua, haya tuoneshe na kitu gani, akionekana kama hana risiti basi yeye ndio atakayetozwa pesa nyingi zaidi kuliko hata zile alizonunua dukani.

Kwa hivyo, napenda tushirikiane kabisa na wafanyabiashara na wananchi wote kwa jumla ili kuhakikisha kwamba tunatii sheria za kuweza kulipa kodi au kuwa na bidhaa zetu na kuweza kuzitunza kwa ajili ya kulipa haki inayostahili ili taifa letu liendelee kuweza kufanya mambo yanayohusika. Maana yake pasipokutozwa kodi basi huduma za mahospitali tutalalamika, za elimu tutalalamika na haya masuala ambayo mheshimiwa anatuwazia mema ya kuongeza mamboya pensheni, kuongeza huduma za jamii hazitafanyika kama hakutakuwa na kodi zitakazolipwa kwa wakati ipasavyo, na kutunisha mfuko ni pamoja na kuwa na nidhamu ya kuweza kulipa kodi ili kila mmoja afanye kazi na aweze kupata haki yake.

Baada ya kusema hayo napenda niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia, na pia kuendelea kumpongeza Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kuendelea kuwaza mambo mengi. Linapopatikana pato kubwa kwa ajili ya nchi yetu, anaendelea kutoa huduma za ustawi kwa jamii. Ahsanteni sana na nawatakieni Ramadhani njema. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo Mhe. Rashid Ali Juma.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi awali ya yote kwanza niwape pole wale wote ambao wamekutwa na msiba ambao tumetangaziwa muda mchache, na Mwenyezi Mungu kwa rehema zake na baraka zake na kama kumi hili linavyoainisha Inshaalah, basi awe amemfisha yule marehemu hali ya kuwa ameachwa huru na moto *Inshaallah* Mwenyezi Mungu amjaalie.

Vile vile sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa fursa hii tena kuendelea kutupa pumzi na sisi kuweza kutumia muda huu basi ili kuweza kuchangia kidogo na kuwapa hususan wananchi wetu ambao wametuchagua, likiwemo Jimbo letu la Amani na wale wengine ambao wanatusikiliza azma hasa ya kuwasilisha miswada hii inayohusiana na masuala mazima ya kodi.

Mhe. Mwenyekiti, napenda nimshukuru Mhe. Waziri wa Fedha nimshukuru kwa kiwango kikubwa kabisa cha uwezo wake umahiri wake, na bado ameendelea kuthibitisha kwamba yeye anahimili kabisa wizara hii na kuisimamia vile inavyopaswa kusimamiwa. Muda mrefu toka alipowasilisha bajeti na hivi sasa anaendelea kuwasilisha hii miswada yetu ya fedha, lakini bado anaonekana kwamba ni mwenye nguvu na naamini ataimaliza miswada yote iliyobakia kwa wakati kama ilivyopangwa. Nakushukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa jitihada zako, unadhibitisha udaktari wako na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akujaalie miaka mitano yote hiyo nafasi uendelee kukaa nayo, ili utuendelezee kutupatia mambo kama haya.

Mhe. Mwenyekiti, sina budi tena kumshukuru Dkt. Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuleta mswada huu wa dharura. Ameuona ni mswada wenye umuhimu na kweli una umuhimu wake. Mhe. Mwenyekiti, mswada huu tunaoujadili hivi sasa kuhusu ushuru wa bidhaa, ni kodi ambayo tulikuwa tunaitarajia muda mrefu sana iwe inafanyakazi ipasavyo. Uharaka huu ulioletwa leo unaainishwa tu ni namna gani ulivyochelewa kutokana na yale mazowea yetu ya nyuma kwamba ushuru huu ulikuwa unasimamiwa na upande wa pili wa Tanzania Bara, kama ulivyoainishwa kwenye katiba kwamba ni moja katika kodi zinazosimamiwa Kimuungano. Lakini ukitizama muundo wake na ukitizama *nature* ile ya Muungano ilivyo. Kwa hivyo kulikuwa kuna uhalali kabisa kuona kwamba mswada huu na aina hii ya kodi inapaswa kutozwa hapa Zanzibar na kusimamiwa na sheria hizi za Zanzibar.

Kwa hivyo kwa Dkt. Ali Mohamed Shein kuliona mapema kwa umuhimu wake huu na kwa bajeti tuliyowekewa safari hii, bajeti yenye kufika *figure* za trilioni moja, basi kunahitajika jitihada za ziada na kuweza kuziibua kodi zote ambazo zilikuwa hazikusanywi vizuri, sasa hivi ziweze kukusanywa ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nikubaliane na mapendekezo yote yaliyokuwemo humu. Nataka nikubaliane na mapendekezo kwamba ushuru wa bidhaa kwa *nature* ya kisiwa chetu, ndio kodi moja ambayo inapaswa kusimamiwa kwa utulivu kabisa. Kama tunavyojua visiwa mara nyingi huwa na milango mingi ya kufanyia biashara, inajulikana wazi kuwa mnapokuwa na visiwa basi uchumi wenu mkubwa hutegemea biashara. Kwa hivyo, tunapofanya suala zima la biashara katika kuipatia serikali mapato, ndio pale inapoonekana umuhimu wa kuvidhibiti vitu ambavyo vina uhalali kwa kuingia kwake, na vina uhalali kwa matumizi yake na vile ambavyo havipaswi kabisa kuingizwa ndani ya nchi yetu.

Kwa hivyo, lengo la ushuru huu wa bidhaa moja ni kuhakikisha kwamba, na hili wananchi wetu walielewe, tunawasilisha kodi hii sio kwa sababu ya kuwaongezea makodi, sio kwa sababu ya kwamba nchi yetu iwe na makodi mengi ndani ya kisiwa hiki hapana. Lakini kodi hii ina malengo ya kuweza kudhibiti vile ambavyo vinapaswa viingie kwa kiwango fulani, vile ambavyo vinakuwa-*discourage* visiingie kabisa, na vile ambavyo vinatakiwa viwe na uangalifu katika kuingia kwake.

Mhe. Mwenyekiti, ukiitizama hii sheria sehemu ya utozaji Sehemu ya Nne, yaani *imposition of the tax* inatueleza vizuri kabisa kwamba lengo la kutoza ushuru huu ni upi na hii ndio sifa ya sheria yoyote ya kodi. Sheria yoyote ya kodi muongozo wake ni lazima iainishe namna gani kodi ile itatozwa. Kwa hivyo, nimefurahika sana kuona kwamba mbali ya kuonesha kuwa kodi hii itatozwa kwa masharti ya sheria hii iliyotungwa, na msimamizi mkuu wa sheria hii ni Kamishna wa Bodi ya Mapato, lakini masharti makubwa yanamsimamia Waziri wa Fedha na Mipango. Napenda ieleweke kwamba Waziri wa Fedha atakayeisimamia sheria hii ni Waziri wa Fedha wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kutokana na hali hiyo basi kuna kifungu cha 5 humu kinachoonesha maeneo ya kuainisha utozaji wa viwango vya kodi. Kuna masharti tunapaswa tuyafuate yale ya Afrika ya Mashariki na Kati, kwa nini. Kwa sababu sheria hii itatawala sana bandarini kwenye uagizaji wa vitu, kwenye utoaji wa vitu na matumizi mengine ya vile vitu pamoja na huduma. Lakini tunapofanya hilo sasa tuelewe wazi kwamba kuna masharti yatapaswa tuyazingatie Kimuungano, yale yatafuata sheria za Kimuungano. Lakini yapo masharti yatapaswa kufuata sheria za Afrika ya Mashariki na yatapaswa yazingatia sheria za Afrika ya Mashariki.

Vile vile ukitizama kiwango cha sheria hii katika kifungu cha 5 na cha 6 bado kuna viwango vinatakiwa kutozwa kwa kufuata *treaty,* mikataba ile ya Kimataifa ya *WTO* kwa sababu gani, mikataba ya Kimataifa inakuwa ina masharti yake inayoeleza kwa nchi zote zinazoridhia namna ya kutoza zile kodi. Kwa hivyo, bado na sheria yetu hii ukiitizama mtazamo mzima wa sehemu ya pili juu ya utozaji wa ushuru huu wa bidhaa na huduma unaelekeza bidhaa gani, huduma gani zinaweza zikafuata viwango vya Afrika ya Mashariki, bidhaa gani na huduma gani zinaweza zikafuata mikataba yetu ya nje na zile ambazo zitapaswa kufuata masharti yetu ya Zanzibar.

Zanzibar yetu hii Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi ilikuwa ikilalamikiwa imekuwa ni *dump* la kuleta vitu vichakavu, vitu vilivyotumika. Lakini sheria hii napenda sana Waheshimiwa Wawakilishi waisome na kuielewa. Pale wanapokuja hapa Barazani tukawa wengi wa kuuliza maswali, tukawa wengi wa kuhoji baadhi ya mambo. Sheria hii sasa imekuja kusimamia zile kero ambazo tunazihisi zimefika hapa kwetu na zinatakiwa kudhibitiwa.

Kwa mfano, unaposema unataka kutoza ushuru wa vitu vichakavu. Nchi yetu hii imejaa sana kama mafriji ambayo yote sio mapya mengi sana ni *second-hand,* ukitizama matelevisheni mengi sana, kila leo ukipita mabarabarani yanatozwa hapa na pale. Kwa hivyo, sheria hii imezingatia sana namna gani ya kuweza kuvidhibiti vile vitu. Kuna vitu vinawezekana kwamba vinaletwa hatujui vina athari za aina fulani. Inawezekana zikaletewa bidhaa za plastiki zikawa na athari za kiafya, tunaweza tukaletewa bidhaa zikiwa za maji maji zikawa za kiafya. Lakini vitu vyengine vinaweza vikaletwa katika uholela wa kuviingiza vikahatarisha hata usalama wa hii nchi.

Mhe. Mwenyekiti, tuseme tunaleta makontena ya mafriji hapa, ndani ya friji unaweza ukaingiza vitu vyenye hatari kabisa, madawa ya kulevya yanaweza yakaingizwa mule, vitu vyenye hatari na usalama wa nchi yetu vinaweza vikaingizwa mule. Kwa hivyo, udhibiti wa sheria hii ukisimamiwa vizuri kama kinavyoeleza kifungu cha 4 mpaka kifungu cha 6 basi kutakuwa kuna mafanikio makubwa. Mimi sina budi kuunga mkono kwa hoja zote za vipengele vilivyokuwemo

humu basi tuone kwamba sheria hii tunaipitisha, tena tunaipitisha kwa nguvu zote kama tulivyozipitisha hizi sheria nyengine ambazo tumezipitisha.

Lakini nifarajike tena na kifungu hicho hicho, kwa sababu mzizi wa kodi hasa ni hii namna gani ya kutoza zile kodi. Napenda wananchi waelewe kwamba, ninapenda sana watu wa Jimbo langu la Amani waelewe kwamba tunatunga sheria hii kwa kuwasaidia wao, mara nyingi tunapoambiwa tulipe kodi za serikali huwa tunahisi kwamba ukiambiwa utowe kodi ya stampu, utowe kodi ya ushuru wa bidhaa, utowe kodi ya ushuru wa *VAT* au *VAT* yenyewe ilivyo ongezeko la thamani, basi tunaona kwamba mtu mmoja amerimbikiziwa yale makodi. Lakini kwa sifa za kodi zilivyo, kitu kimoja au bidhaa moja inaweza ikatozwa aina nne za kodi. Kwa hivyo, kuja kwa ushuru wa bidhaa hapa kutaainisha kwamba kuna vitu vitatakiwa vitozwe kodi, lakini sio kuongeza kodi. Kwa hivyo, wananchi wetu na waheshimiwa wetu wanapaswa kulielewa hili, hatuna lengo hapa la kusema kwamba tumeongeza wingi wa kodi, lakini tuna uwezo wa kusema serikali inaweza ikapata mapato yake kwa kupitia huu ushuru wa bidhaa.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niwatanabahishe sana wananchi wanaotusikiliza tunavyoipitisha sheria hii, vile vile niwatanabahishe sana Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu kuzisoma sana hizi sheria. Hii ni sheria ambayo inaweza ikakuza kiwango kikubwa sana cha mapato endapo tutaipitisha na tumuombe tena na Rais bado aisaini kwa haraka sana ili iweze kutumika muda mchache ujao.

Mhe. Mwenyekiti, ukitizama kifungu cha utozaji wa kodi, kifungu cha 5 na kifungu cha 6 kinaeleza namna gani sheria hii inaweka majadweli ya kutozea kodi. Ukitizama biashara nyingi zinazofanywa katika uwekezaji. Nchi yetu hii sasa hivi imekuwa ikiagiza vinywaji vya aina nyingi sana. Hapo nyuma tulikuwa tunapata tatizo sana namna ya kutoza vinywaji, lakini ukitizama jadweli la kwanza, wananchi napenda sana waitizame hii sheria, waisome na waifahamu na wenzetu Waheshimiwa Wawakilishi hapa napenda sana muzitizame hizi jadweli, hizi zinaeleza wazi namna gani mapato wingi wake unatakiwa kukusanywa na namna gani mapato yanapoweza kupotea tunaweza tukayakisia mapato yaliyopotea.

Mhe. Mwenyekiti, ukitizama hili jadweli, kwa mfano jadweli la kwanza linaelezea namna gani ya vinywaji vinavyotakiwa kuingia hapa nchini. Sisi sio wazalishaji wengi wa vinywaji, lakini ndani ya nchi yetu. Napenda kunukuu yale maneno ya Mhe. Abdalla Ali Kombo, alisema siku moja hapa kwamba kule kijijini kwao Kenge haliwi, lakini ndani ya nchi hii muna Kenge wengi sana. Ni sawa sawa na hii sheria inavyoonesha kwamba tumeitunga hii katika *schedule* moja namna gani ya kutizama tuvitoze kodi vinywaji vinavyoingia hapa nchini. Wenyewe hatuzalishi vinywaji vingi, tuna nafasi nzuri sana ya kutumia matunda na vitu vyengine, lakini sio wengi wa kuzalisha *juice* na mambo mengine ya vinywaji yanayotokana na matunda hayo. Lakini Zanzibar tumekuwa na bahati sasa ya uagiziaji wa vitu hivyo.

Waheshimiwa Wawakilishi napenda sana wangeiona fursa iliyotumiwa katika kuleta sheria hii vinaelezwa wazi vinywaji vinavyoingia hapa nchini namna gani vinapaswa kutozwa kodi kutokana na zile *schedule* ambazo zimeelezwa hapa. Nimefarajika kuona kwamba lita moja ya vinywaji ambavyo ndani yake vina zabibu kwa kila lita vinatakiwa vikusanywe ushuru huu shs. 2,236/= angalia chupa ya lita moja zinapoagiziwa hapa zikiwa ndani ya kontena nzima zinaingia

Kiwengwa, zinaingia Nungwi, zinaingia na sehemu nyengine ni kiasi gani cha kodi kinapaswa kutozwa hii ni sehemu ya kuiagizia tu ile lita moja ya kile kinywaji. Baadae kuna sehemu nyengine ya kuitoza pale inapouzwa kila inapokwenda hatua kwa hatua ushuru wa ongezeko la thamani anayeuza ambae hakusajiliwa kwenye kodi nyengine za ushuru wa bodi ya mapato kutoza zile kodi za ongezeko la thamani bado anaweza kutozwa ushuru wa stempu, kwa hivyo nataka kuonyesha kwamba bidhaa moja kuongezewa kodi hii ya ushuru wa bidhaa itaonyesha manufaa makubwa kwa Serikali yetu.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nisiwe mwingi wa kusema mengi kabisa nataka nizidi kuendelea kupongeza sana kuwepo kwa sheria hii lakini nataka nieleze wazi kwamba tuna kazi nzito katika kuvisimamia hivi vifungu ambavyo tutavipitisha leo. Kutunga hii sheria sio kazi kubwa sana kazi kubwa ni usimamizi wa hizi sheria. Nafurahia sana namna gani hizi sheria zilivyoweka adhabu, adhabu tunapoweza kugundua kwamba hiki hakijalipiwa kodi adhabu yake ikoje, hiki kimekwepa kodi adhabu yake ikoje. Kwa hivyo na mimi naendelea kumuomba Mhe. Waziri wa Fedha kwamba Serikali nayo iendelee kama tulivyoweka misimamo yetu kusimamia vizuri zaidi namna gani ya kuweza kukusanya hii kodi bila ya kupotea aina yoyote. Lakini kwa kupitisha kodi hii basi Mwenyekiti, nataka nikuthibitishie wazi kwamba sura na muangaza dira inaonekana kwamba ile bajeti ambayo tumeiweka sasa inaweza ikafikiwa.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana naunga mkono hii hoja kwa asilimia mia tuipitishe kwa uwezo wetu wote na wananchi wakaweze kutoza hizi kodi na zisimamiwe ipasavyo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na michezo kwa mchango wako sasa naomba nimuite Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa ajili ya kufanya majumuisho ya hoja zilizotolewa na wajumbe.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kuwashukuru Waheshimiwa wajumbe wote waliopata fursa ya kuchangia Mswada wa Sheria hii ya Ushuru wa Bidhaa na nianze kwanza kwa kumshukuru sana Mhe. Zulfa Mmaka Omar wa viti maalum aliyetoa taarifa ya kamati, Kamati ya bajeti lakini niwashukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya bajeti na Makamo wake na Wajumbe wote kwa kweli waliufanyia haki sana Mswada wa Sheria hii, tulikuwa pamoja na walipitia kifungu kwa kifungu na walitoa maoni yao na maoni yao hayo yatazingatiwa kikamilifu.

Lakini pia nimshukuru sana Mhe. Rashid Makame Shamsi wa Jimbo la Magomeni nae kwa kutoa michango yake lakini pia kuainisha maeneo ambayo bado yapo yana matatizo ya *typing mistake* na nimwambie tu Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati baadhi yake wameyaona lakini yako maeneo mengine ambayo nao wameyaona na tunayachukua. Nimueleze tu Mhe. Rashid nchi washirika kama alivyozungumza tunazozitambua ni kwa mujibu wa *East Africa Community Treaty* ya mwaka 2004 iliunda tena Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Lakini kuna masuala aliyazungumza Mhe. Rashid Makame Shamsi ya tafrisi ya chombo naomba hili tulichukue na tutalifanyia kazi lakini pia alizungumzia kuhusiana na kifungu cha 82(2)(c) lakini hichi nimueleze tu wakati Wajumbe Waheshimiwa wa kamati wanapitia Mswada huu kifungu kidogo cha (2) kilifutwa kwa hivyo sasa hakipo.

Lakini kwenye kifungu cha 13(1)(c) tunakubaliana nae na ushauri wake tunauchukua. Alizungumzia suala la kuweka mwaka katika sheria ya *Custom* ya Afrika ya Mashariki, *East Africa Community Management ACT* tunalipokea na tutaweka mwaka kama ulivyopendekeza, lakini pia tume-*note* katika kifungu cha 22, lakini kifungu cha 27na 28 kwa bahati nzuri Kamati ya Bajeti imetufanyia marekebisho.

Kuna suala ambalo lilizungumzwa na Mhe. Rashid Makame Shamsi na naomba nimtoe wasiwasi kwamba hakutokuwepo na mgongano wala msongamano baina ya sheria hii na hii sheria ya ushuru wa bidhaa sura ya 147 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kabla ya kuja na Mswada wa Sheria hii kulifanyika mawasiliano ya kutosha baina ya Wizara zetu mbili lakini pia mazungumzo haya yalihusisha Afisi za Wanasheria Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar nao wameridhika kwa sababu hayo ni matakwa ya kikatiba. Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 katika jadweli la kwanza mambo yaliyowekwa kama masuala ya Muungano ni pamoja na ushuru wa bidhaa, ushuru wa bidhaa kwa bidhaa zinazozalishwa nchini. *Local Manufacture Goods,* sasa utaiona kulikuwa na mwanya kwa sababu bidhaa zinazoingizwa nchini hazikuwekewa utaratibu wa kisheria.

Lakini vile vile kukua kwa huduma mbali mbali zinazotolewa katika nchi yetu nayo hiyo pia sheria ilikuwa *silence* sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini vile vile tulikuwa hatuna sheria kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa hivyo kinachofanyika hapa sasa ni kuziba mwanya ule uliokuwepo na ndio maana tunakuja na Mswada wa Sheria hii. Lakini kodi hizi niseme kuwa zilikuwa pia zikitozwa kwa huduma mbalimbali, ikiwemo huduma za mawasiliano ya simu ilikuwa ikitozwa huduma za fedha zilikuwa zikitozwa, lakini ilikuwa ikitozwa na haya mashirika yalikuwa yakilipia Serikali ya Jamhuri ya Muungano bila ya fedha zile kupatikana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa sababu hakukuwepo na *instrument* na baadhi ya mashirika haya yalikuwa yanatuambia kwamba tunapozidai pesa hizo wanasema *instrument* ipi mnayodaiya, kwa sababu *instrument* iliyokuwepo ni ile ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hivyo tumekubaliana kwamba hilo tuliweke sawa kwa hivyo hakutokuwepo na ongezeko la kodi wala hakuna kodi mpya ni kodi ile ile na uzuri kwamba tumekubaliana kuweka viwango sawa baina ya Zanzibar na wenzetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kusaidia kuimarisha biashara baina ya pande mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa hivyo wafanya biashara wasi na hofu kwa sababu kodi hii walikuwa wakitoa walipa kodi wetu walikuwa wakitoa na wananchi ndio wanaolipa na kwa sababu hizo basi inalipwa na inaendelezwa lakini kilichofanyika ni kuweka utaratibu mzuri zaidi wa ukusanyaji wa kodi hiyo. Kwa hivyio nimtoe wasi wasi hakutokuwa na ongezeko wala si jambo jipya, lakini kilichowekwa hapa ni utaratibu wa kisheria.

Lakini vile vile nimtoe wasiwasi kwamba huduma zile zitakazotozwa ushuru wa bidhaa ni pamoja na huduma za mawasiliano ya simu ambazo sasa tunaendelea kukatwa pesa hizo kwa sababu ukipiga simu hizo fedha zinakatwa. Lakini vile vile malipo ya kuangalia TV za *Satellite*, televisheni nazo sasa tutaanza kulipa lakini hizo pesa zitakuwa zinaingia kwenye Mfuko wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na huduma za fedha. Lakini kuna jambo ambalo la faraja

zaidi Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hivi karibuni alizindua mfumo wa ukusanyaji wa kodi kwa miamala inayofanyika kielektroniki, kwa maana ya *Electronic Revenue Collection System* na mfumo huo uliandaliwa kwa pamoja baina ya *ZRB* na *TRA,* kwa hivyo sasa kwa huduma za simu fedha zile zinazohusika kuingia kwa upande wa Zanzibar zinaingia moja kwa moja katika *account* za *ZRB*. Mfumo ule unatakiwa kufanyiwa kazi zaidi ili pia kuingiza miamala inayotokea katika sehemu nyegine ikiwemo mabenki kwa maana ya huduma za kifedha zinazotolewa kupitia Taasisi hizo za kifedha.

Mhe. Mwenyekiti, lilikuwepo na suala jengine la Mhe. Raishid Makame Shamsi kifungu cha 31 cha adhabu alisema kwamba adhabu ya kifungu cha 31 ni kidogo na kina tofauti na kile cha 31(2) na hii inatokana na sababu kwamba adhabu inatolewa kwa mujibu wa uzito wa kosa lenyewe, sasa kifungu cha 31(1) adhabu ni ndogo kwa sababu makosa yaliyoainishwa pale ni makosa ya kawaida. Lakini ukenda kwenye 32(2) kwamba kosa lenyewe ni kubwa kwa hivyo adhabu yake ni kubwa inahusisha udanganyifu, sasa ikihusisha udanganyifu kwa maana hawa watu wamefanya udanganyifu na adhabu yake inabidi istahiki kama uzito wa kosa lenyewe lililofanyika. Lakini kwa jumla yale yote aliyoyaona nimhakikishie kwamba tumeyachukua na nimshukuru sana kwa sababu *observation* zake kuna baadhi ya maeneo sisi na Wajumbe wa Kamati hatukuyaona kwa hivyo tunayachukua na tutayafanyia kazi.

Mhe. Shehe Hamad Matar Mwakilishi wa Jimbo la Mgogoni yeye alizungumzia zaidi masuala ya uadilifu alitoa pongezi kwa Mhe. Rais naamini pongezi hizo zitafika kwa Mhe. Rais, lakini vile vile alizungumzia suala la watendaji wetu hasa wa bandarini na mimi nikubaliane nao kwamba bado wapo watendaji ambao sio waaminifu sio bandarini tu katika maeneo mbali mbali ya ukusanyaji wa kodi. Kwa sababu mambo haya yanayoshughulikia mambo ya kifedha haya yana ushawishi wake na kila mtu na uwezo wake wa kustahamili ushawishi ndio maana tunaweka sheria hizi, sasa kwa wale ambao watashindwa kuzizuia nafsi zao na vishawishi vinavyotokana na pesa basi sheria hizi zichukue mkono wake. Sasa kitakachofanywa ni kuzisimamia kwa ukamilifu kuafuatilia na hilo niwaahidi kwamba katika maeneo yote ya vyanzo vya mapato yetu ya ndani sisi tumejipanga kufuatilia kikamilifu na tutaendelea kutoa taaluma kwa watendaji wetu ni jambo muhimu sana.

Hivi sasa tumepanga baada ya kupitishwa bajeti ya Serikali ya mwaka ujao wa 2017/2018 tutafanya mikutano na watendaji wote wanaohusika na masuala ya fedha wakiwemo ma-*cashier* na wale wanaokusanya fedha, tutawafahamisha vizuri na tutawafahamisha hatari itakayomkabili yule atakayekataa kubadilika. Kwa hivyo hilo litakalokuja kutokea wale wasiwe na sababu tena ya kuwalalamikia watu itakuwa ni makosa yao wenyewe, utaratibu unaandaliwa wa ufuatiliaji mzuri zaidi na kuhakikisha kwamba wale wote wanaohusika na masuala ya ukusanyaji wa mapato wanafanya kazi zao kwa uadilifu mkubwa. Hilo Mheshimiwa nakuomba usiwe na wasiwasi nalo.

Mhe. Omar Seif Abeid yeye alizungumza mengi na mengi yao ni michango ambayo nimueleze tu Mhe. Omar tunaichukua na pia lile suala lake alilolizungumza la kifungu cha 22 kwa maana ya uwezo yeye alisema kwamba tubadilishe kwa kuweka neno cheo, sasa hapa ni Mwanasheria Mkuu atatusaidia lakini suala la uwezo ndilo linalotumika mara nyingi sana katika Miswada ya Sheria na katika Sheria mbali mbali linatumika neno uwezo na huo uwezo unatokana na hicho

cheo chenyewe, kwa sababu kile cheo ndio kinachotoa uwezo wa afisa anayehusika na utekelezaji wa kifungu chochote kile cha Sheria. Kwa hivyo mimi bado namshawishi Mhe. Omar Seif Abeid tukubaliane kwamba twende na kubaki kuwa na neno hili hili la uwezo badala ya kutumia neno cheo.

Maoni yake mengine tumeyachukua lakini pia alikuwa na maoni ya kifungu cha 31(e) na (f) na hapa alizungumzia kwamba kushindwa kujibu masuali na atatiwa hatiaani kwenye kifungu (e) na (f) lakini niseme tu kwamba hatotiwa mtu hatiani mpaka ahusishwe na ithibitike kwamba ametenda kosa kwa maana kuwe na *Conversion* baada ya kutokea hilo *Conversion* ndio huyo mtu anatiwa hatiani kwa hivyo pia namuomba na yeye asiwe na wasiwasi.

Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana sana Mhe. Moudline Cyrus Castico Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto na yeye amechangia vizuri sana Mswada wa Sheria hii nampongeza sana na namshukuru kwa kutoa ufafanuzi pia katika baadhi ya maeneo.

Lakini pia nimshukuru sana sana Mhe. Rashid Ali Juma Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa kweli yeye ni mdau mkubwa sana katika masuala ya kodi na huko nyuma amewahi kufanyia kazi chombo hichi muhimu cha kodi za wananchi, mambo mengi amesaidia wakati huo na hivi sasa anaendelea kutusaidia sana katika ushauri na maoni mbali mbali anayotupatia na mahala ukishapita basi rekodi yako inakuwepo. Kwa hivyo na yeye bado ni mwanachama wa suala la kodi kwa sababu amekitumikia sana sana chombo hichi na hasa alikuwa Meneja pia wa kutoa elimu kwa walipa kodi. Kwa hivyo anavyolizungumza Mhe. Rashid anakielewa na namshukuru sana sana kwa ufafanuzi alioutoa.

Mhe. Mwenyekiti, maoni yaliyotolewa yote ni ya jumla na naona sina haja ya kueleza zaidi kwa sababu yaelekea pia Waheshimiwa Wajumbe wameufahamu sana Mswada huu wa Sheria na hasa pale tulipokuwa tumeuzungumza kwa umakini sana wakati tulipofanya semina hivi juzi. Kwa hivyo baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mweyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Khalid Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na imeungwa mkono, sasa naomba niwahoji wanaokubali na hoja hiyo, wanaokataa waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama kamati ya kutunga sheria ili kuupitia Mswada huu kifungu kwa kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa na Huduma ya mwaka 2017

Sehemu ya Kwanza

Utangulizi

Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 2 Matumizi
Kifungu 3 Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu 4 Utozaji wa Ushuru wa Bidhaa na Huduma Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 5 Uainishaji wa Kiwango Cha kutoza Ushuru kwa Bidhaa zinazoingizwa Nchini Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 6 Kiwango cha Kutozea Shuru kwa Huduma Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 7 Ukaguzi wa Kumbukumbu Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 8 Muda wa Usambazaji na Utozaji wa Ushuru kwa Huduma na Uingizaji wa Bidhaa Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 9 Udhibiti wa Bidhaa zinazotozwa Ushuru Pamoja na Mrekebisho yake
Kifungu 10 Eneo la Usambazaji wa Huduma Zinazotozwa Ushuru Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 11 Kukasimu Kazi na Majukumu Pamoja na Marekebisho yake.

Sehemu ya Tatu

Malipo ya Ushuru

Kifungu 12 Malipo ya Ushuru
Kifungu 13 Mtu Anayewajibika Kulipa Ushuru Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 14 Kugomboa Ushuru Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 15 Watu na Taasisi zinazosamehewa Kulipa Ushuru Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 16 Misamaha ya Ushuru kwa Bidhaa Zinazoingizwa Nchini kwa Ajili ya Kupelekwa Nje ya Nchi Pamoja na Marekebisho yake
Kifungu 17 Misamaha kwa Bidhaa Zinazobakia Kwenye Chombo
Kifungu 18 Misamaha kwa Bidhaa Zilizolipiwa Ushuru Tanzania Bara Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 19 Marejesho ya Ushuru Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 20 Malipo ya Marejesho ya Bidhaa Zilizoharibika Pamoja na Marejesho yake.
Kifungu 21 Marejesho ya Ushuru

Sehemu ya Nne

Hesabu na Kumbukumbu

Kifungu 22	Hesabu na Kumbukumbu
Kifungu 23	Kuingiza Bidhaa ya Nchi kwa Mara ya Pili Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 24	Udhibiti wa Forodha kwa Bidhaa Zinazopaswa Kutozwa Ushuru Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 25	Uingizaji na Uhifadhi wa Bidhaa Zinazotozwa Ushuruu Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 26	Bidhaa Zinazochukuliwa Kuwa Zimeingizwa Zanzibar Pamoja na Marekebisho yake
Kifungu 27	Wajibu wa Kulipa Ushuru wa Bidhaa na Huduma kwa Mtu Aliyekuwa Hayupo Pamoja na Marekebisho Yake.
Kifungu 28	Ukwepaji wa kulipa Kodi Pamoja na Marekebisho Yake
Kifungu 29	Wajibu wa Kulipa Ushuru wa Huduma na Bidhaa Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 30	Kujifananisha.
Kifungu 31	Makosa na Adhabu.
Kifungu 32	Makosa Mengine Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 33	Adhabu ya Jumla Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 34	Kanuni Pamoja na Marekebisho yake.
Kifungu 35	Kubakiza Pamoja na Marekebisho yake.

Sehemu ya Sita

Marekebisho Yatokanayo

Kifungu cha 36	Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi Nam. 7 ya 2009.
Kifungu cha 37	Marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mapato ya Zanzibar Nam. 7 Mwaka 1996.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia Mswada wangu kifungu kwa kifungu na kukubali pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe**.** Mwenyekiti**,** naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri, Hoja imetolewa sasa naomba niwahoji wanaokubali, wanaokataa, wanaokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa na Huduma ya Mwaka 2017

(Kusomwa mara ya tatu)

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa na Huduma ya Mwaka 2017. Usomwe kwa mara ya Tatu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri, Hoja imetolewa sasa naomba niwahoji wanaokubali, wanaokataa, wanaokubali wameshinda.

Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru sana lakini kabla ya kuahirisha na mimi nachukua fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar kwa kutuletea Mswada huu. Lakini pia naomba nimpongeze Waziri wa Fedha na Mipango na Waheshimiwa Wajumbe wote waliochangia pamoja na Kamati ya Bajeti.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango nadhani kwa umahiri wako na kwa vile wachangiaji wengi wameunga mkono kwa asilimia mia Mswada huu, kilichobaki sasa mbele yako ni kuufanyia kazi. Nina imani utafanya kazi ipasavyo kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar.

Waheshimiwa Wajumbe naomba kuakhirisha kikao chetu hichi leo mpaka kesho saa 3:00 asubuhi.

(Saa 7:04 mchana Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 22/06/2017 saa 3:00 za asubuhi)